

# *KUMTENDEA MUNGU KAZI BILA MAPENZI YAKE*

 Hebu tuendelee kusimama sasa tunapoomba. Na tuinamishe vichwa vyetu.

<sup>1</sup> Bwana, tuna furaha asubuhi hii kurudi nyumbani kwa Mungu kwenye ibada nyingine. Na tunaomba Mungu kwamba utatusahihisha asubuhi hii makosa yetu yote. Tuonyeshe njia zile ulizochagua zitupasazo kupidia, na tupe Neema Yako na upendo, ili tupate kufuata njia zile na maagizo kwa moyo wetu wote, ili tuonekane siku ile katika Kristo, bila lawama, kwani tunaamini, Bwana, kwamba kufunuliwa Kwake ku karibu.

<sup>2</sup> Tunaona ishara zote alizonena zitatokea kabla tu ya kuja Kwake sasa zikitimia. Na kwa furaha tunatazamia muda huo. Kama Ibrahim wa kale alivyomtazamia yule mwana wa ahadi, na kuona zile ishara za mwisho za Mungu zikishuka ulimwenguni, hapo alijua kwamba haitachukua muda mrefu hadi huyo mwana atokeapo. Na sasa twaliona hilo likirudia tena. Yesu alituambia kwamba wakati mambo haya yaanzapo kutokea tuinue vichwa vyetu, kwamba ukombozi—ukombozi wetu unakaribia: mshangao wa wakati huo, dhiki kati ya mataifa, matetemeko ya nchi mahali mahali, bahari ikivuma, na moyo wa mwanadamu ukikoma kwa hofu.

<sup>3</sup> Nasi twatambua kwamba tuko katika saa hiyo wakati ambapo mataifa hayajui la kufanya. Inaonekana vita vingine vinakuja. Hicho kingekuwa kitu kibaya jinsi gani. Dunia ikivunjika-vunjika, wanasyansi walisema kwamba kitu cha kutisha kiko karibu. Tunaona Biblia ikinena juu ya jambo hili. Basi, Bwana, tusaidie leo kusimama katika hii nyumba ya kusahihishwa, na kutii amri kutoka kwa Mungu wetu kusonga mbele katika saa hii ya giza kuangaza Nuru, kwani huenda ikawa nafasi yetu ya mwisho kufanya hivyo. Kwani twaomba hili katika Jina la Yesu na kwa ajili Yake. Amina. (Ketini.)

<sup>4</sup> Hakika naona hii kuwa ni heshima kuu kuwepo hapa katika maskani asubuhi hii. Na samahani kwamba hatuna nafasi yenu ya kuketi hapa. Na mahali hapa pamejaa watu, na wamesimama kila mahali kule nje... Ninyi watu mliopo nje sasa, mwaweza kusikia hili katika redio zenu, nasahau... [Ndugu Neville anamwambia Ndugu Branham ni katika mita bendi ngapi yaweza kusikika—Mh.]... 55 hadi 57. Ninyi watu mliopo nje na katika sehemu za kupaki magari na barabarani, mwaweza kusikia hili katika redio zenu kati ya 55 na 57 katika bamba la redio zenu.

<sup>5</sup> Kwa hiyo tumejaribu... Nalikuwa nikirudi, hasa, kwa—hapa kujaribu kufanya mkutano wa kama siku kumi kuzungumzia juu ya somo la vile Vitasa Saba vya Mwisho; kwani kati ya Vitasa vile ni zile Baragumu. Na nilikuwa nikiwaambia katika ule—wakati nilipokuwa ninakwenda kuhubiri juu ya zile Baragumu Saba, kwamba nitavileta pamoja vile Vitasa na yale Mapigo. Na nalifikiri ingekuwa wakati mzuri, nilikuwa nimerudi tu kutoka Afrika; na—na watoto hawakuwa wamepata likizo yao. Mtoto wangu mdogo wa kiume, Joseph, amekuwa—amekuwa akiendelea—anahitaji wiki chache za kujifunza juu ya kusoma kwake. Alifuzu haidhuru, lakini hakufikia wastani, kwa hiyo tulimwacha Tucson hivyo—wakati nilipokuwa Afrika, na aliendelea na kusoma kwake na kufaulu kwa kisomo cha shule ya mchana. Kisha tulirudi. Basi nalifikiri, huku watoto wakiwa likizoni nitafanya mkutano mdogo hapa na watu na kuhubiri masomo haya. Lakini basi tulipofika hapa, tuliona kwamba hatungeweza kupata ukumbi wa shule.

<sup>6</sup> Na naliuju maskani hayatakuwa yanatosha kuwaketisha watu na kuwfanya wastarehe inavyowapasa wakati wao—ninapokuwa na ujumbe huu; kwa hivyo, ilitupasa ku—kufanya mpango tofauti. Na badala ya kuwa na zile—zile siku kumi ambazo tulikuwa tukipanga kuwa nazo; vema, nilifanya ibada mbili tu kwa kila Jumapili—Jumapili hii, Jumapili ijayo, na Jumapili ifuatayo, ibada mbili, ili kwamba... Nasi hatukuitangaza. Na kisha, kama ye yote alisikia kwa njia yo yote ya kwamba mikutano itaanza tarehe ishirini na nane kwenye ukumbi wa shule, kama Mungu angeruhusu, vema, kama mna rafiki wo wote na mmekodisha vyumba vyo vyote kwenye vyumba vya kulala, ni—ningefutilia hilo mbali (waona?), kwa sababu ina—kwamba wao—hatuwezi kuupata kwa urahisi; hawawezi kupata ule—ule ukumbi wa shule.

<sup>7</sup> Na sasa, nataka kuzungumza juu ya—ibada tu za kiinjilisti Jumapili asubuhi. Na Jumapili usiku nataka niwe na maombi kwa wagonjwa. Na tunatumaini kwamba Mungu atakutana na ninyi watu mlion wagonjwa. Sijui Billy atawashughulikia jinsi gani, nafikiri, kutoa kadi za maombi, au namna zo zote kulisimamia kusanyiko. Lakini tutafanya yo yote tuwezayo kufanya kumuombea kila mtu katika hizi wiki tatu zijazo ambazo tunakusudia kuwa na ibada, kama ni mapenzi ya Bwana.

<sup>8</sup> Na kisha, mara nyngi kuna mahojiano ya kibinagsi, mtu fulani anataka kukuona kwa dakika moja juu ya jambo fulani au jambo kama hilo. Nasi tuta... Ni wangapi hapa wanataka mahojiano ya kibinagsi, hebu tuone mikono yenu. Ala! Nani asiyependa?

<sup>9</sup> Kwa hiyo basi, tuna... Yaonekana itakuwa vigumu kuyapata, kwa hiyo andikeni matakwa yenu na muyatume—pelekeni kwa Billy, kisha nitayapata kutoka huko. Na sasa,

atatangaza kuhusu—nakisia, kadi za maombi, kila zinapopaswa kutolewa.

<sup>10</sup> Ni wangapi wa ndugu zetu wanaohudumu walio hapa asubuhi hii. Hatukuwa na nafasi ku...sidhani...mmemtambua ye yote wao? Kuna wahudumu wangapi hapa asubuhi hii? Tafadhalini inueni mikono yenu juu tu, au msimame. Hebu tuone ni wahudumu wangapi walio katika kusanyiko asubuhi hii. Vema, vizuri! Bwana ashukuriwe kwa watu hawa. Laiti tungelikuwa na muda wa kufahamiana na kila mmoja wao, lakini nina hakika mnawaona nasi—Mungu anawajua katika huduma yao; na tunaomba kwamba Mungu awabariki sana. Bila shaka wengi wao wamefunga ibada zao kuwepo hapa.—Ndugu Junior Jackson, na nadhani, Ndugu Don Ruddell. Na matangazo haya yanakuja katika makanisa yao. Na katika—pia kule New York na mahali pengine katika taifa hili ni kwa simu za kibinafsi katika kila kanisa asubuhi hii.

<sup>11</sup> Ninafurahi kumuona Ndugu Richard Blair akiteti hapa. Nilisoma hivi karibuni tu barua kuhusu jambo kuu ambalo Mungu alilitenda mionganoni mwa watu kule. Hivi majunzi, kama ninavyoolewa (Naweza nikosee, Ndugu Blair; kama nimekosea, nisahihishe), alikuwa akifanya kazi, akimsaidia mtu kuwekea gari waya au kitu fulani, naamini ilikuwa hivyo. (Nalisoma barua ile.) Na waligeuza kitu fulani; na hata hivyo, ilichukua umeme hadi kwenye maji ambapo m—mtoto mdogo wa kiume alikuwa (mmojawapo wa—mtu yule aliyekuwa mwenye gari lile, mtoto wake mdogo wa kiume, kijana tu mdogo, na lilimuua yule mvulana mdogo. Na tumbo lake lilivimba na...Twajua mshtusho wa umeme, hicho ndicho—wanapokufa hicho ndicho kinachotokea. Akakondoa macho yale madogo; meno yake yakaumana.

<sup>12</sup> Liliwatisha wandugu vibaya sana. Ndugu Blair alisema aliwazia angeweza kunipata mahali fulani kumuombea, lakini alikumbuka kwamba ilikuwa kwamba “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa ajili ya Jina Langu, nami nipo papo hapo katikati yao.” Na yule baba alichuna vidole vyake akijaribu kuingiza vidole vyake katika kinywa cha mvulana yule akifungue. Kisha walipiga magoti wakaanza kumuombea mvulana yule mdogo, naye akapata uhai wake tena.

<sup>13</sup> Hilo ilikuwa kweli, Ndugu Blair? Mmoja wa ndugu zetu waaminifu hapa. Lo, huyo kijana mwanamume yuko hapa. Vema, Bwana ashukuriwe! Hilo ni zuri. Tungependa usimame, mvulana Sonny. Sasa, tunashukuru Bwana wetu mpenzi kwa hili. Huyo ni baba wa mvulana yule mdogo? Wewe ndiwe baba? Hilo ni sawa. Na hapo yupo Ndugu Richard Blair. Mungu wetu aweza kufanya kitu cho chote. Ndiyo, bwana. Aliliahidi. Tunaishi katika Uwepo wa Mungu yule mkuu, wa utukufu, Baba wa mbinguni. Na mambo yote ambayo sisi—yanawezekana kama twaweza tu kuliamini.

<sup>14</sup> Mnaona kile hilo hufanya, ilivyofaidi maisha ya mtu yule kuamini hilo? Liliokoa mvulana wake mdogo. Sasa, Mungu alikuwa na watumishi Wake waaminifu hapo ku—Ndugu Blair na wao—kuombea mvulana yule mdogo alipokuwa katika hali ile. Ndiyo, kitu cho chote kinapotokea, kumbuka, ninyi ni watoto wa Mungu aliye Hai. “Walipo wawili au zaidi wamekusanyika katika Jina Langu, nipo hapo.” Na tena imeandikwa: “Yeye ni msaada utakaonekana tele wakati wa mateso.” Na kama pamewahi kuwa na matatizo, mvulana yule mdogo akiwa amelala pale amekufa ardhini kutokana na mshtusho wa umeme uliompitia . . . Kwa hiyo, tunamshukuru Mungu asubuhi hii kwa miyo yetu yote kwa hizi—kwa mambo haya ambayo ametenda kwa ajili yetu.

<sup>15</sup> Mungu awabariki watu hawa waaminifu pia. Katika wakati wa dharura huo ndio muda wa kumtafuta Mungu; na kumtazamia Yeye na muwe rafiki Zake kabra ya dharura kuja. Twajua hili: Kama tunampendeza Mungu, twaweza kumuomba kitu cho chote, kama ambavyo ungemuomba rafiki mwagine ye yote; na Yeye ni msaada utakaonekana tele wakati wa mateso.

<sup>16</sup> Nilikutana hivi jana tu huko barabarani na dada wa Ndugu John Martin. Nilikuwa . . . Mtu mmoja alikuwa amenisimamisha huko barabarani na mtu mwagine alipita karibu na akanipungia mkono wake. Wakati wa kurudi nyumbani, mnajua, unawaona watu kila mahali wakisimama na kupeana mikono na kadhalika. Na bibi huyu, nakumbuka waliniita hivi majuzu ambapo mtu fulani alimgonga nyuma katika gari dogo na akapasua uti wake wa mgongo na kadhalika juu chini. Ilikuwa apooze maishani mwake mwote. Anaketi mkutanoni asubuhi hii akifurahia Uwepo wa Mungu. Nalikuwa tu nikizungumza naye chumbani mle; nataka kuomba pamoja naye tena, naye alikuwa . . . Yupo hapa mahali fulani. Nakisia hakuweza kurudi ndani. Lakini hapa! Hakika, yupo hapa akiketi papu hapa nasi. Hilo ni sawa. Hebu simama kidogo tu, Dada, ili watu waweze . . . Yupo hapa bibi huyo ambaye daktari alisema siku chache zilizopita hatatembea kamwe, aliyepasukiwa na uti wa mgongo na kila kitu kutokana na mgongano—mgongano; na hapo anasimama, mzima. Unajua Biblia ilisema, “Nao hawakuwa na neno la kujibu, sababu yule mtu alikuwa akisimama kati yao.” Hilo ni sawa. Hapa yupo kijana mdogo aliyefufuliwa, na hapa pana mwanamke mwenye uti wa mgongo uliopasuka wakisimama kati yetu. Imeisha fanyika tu. Kwa hivyo Yeye ni yule jana, leo, na hata milele. Na libarikiwe Jina la Bwana! Jinsi itupasavyo kufurahi kwamba tunaishi sasa katika uwepo Wake na kujua kwamba Yeye ni huu msaada upatikanao wakati wa mateso.

Nina furaha kumuona Ndugu Vayle, Ndugu Martin, wengi sana wakiwepo asubuhi hii. Na Bwana awabariki sana ninyi ndugu.

<sup>17</sup> Sasa, ni . . . najua si baridi humu kwa umati huu wote, hata hivyo, nilipoondoka Tucson hivi majuzi, joto likuwa kama mia moja na nne au tano; na yapata usiku wa manane ilikuwa tisini na tatu, na basi naona hili ni zuri sana kwangu. Kisha huko Parker walisema likuwa mia moja na arobaini Ijumaa kabla hatujaondoka. Na waweza kufikiri jinsi ilivyokuwa joto. Bila shaka hiyo ni jangwani.

<sup>18</sup> Na sasa, hizi Jumapili tatu zijazo . . . Leo, tarehe kumi na tano, naamini, hilo ni sahihi, au kumi na sita? Kumi na tano, siyo? [Mtu fulani anajibu, “Kumi na nane”—Mh.] Kumi na nane. Na ishirini na nane na A—Agosti moja. Ni sawa? [Mtu fulani anajibu, akitoa tarehe sahihi—Mh.] Ishirini na tano—kumi na nane, ishirini na tano—na tarehe ya kwanza kutakuwa na ibada kwenye maskani. Msialike, mnajua, msialike wengi kupita kiasi sababu, mnaona, hatuwezi kuwaweka walio ndani—walio nije hapa ndani sasa, mwajua, na inazidi kuwa baya. Rudini tu mkiweza.

<sup>19</sup> Na—na kisha nipo hapa kuwakusanya wadhamini pamoja. Yaonekana ninavunjwa na huku kukatazwa kwote kwa mahali pa kufanya mkuutano wakati ninajisikia kuongozwa kuufanya. Kwa hiyo nitakwenda kuwaomba kama hatuwezi kuchukua hema letu na—na kulismamisha na kukaa pale tu, na, mwajua. Kuenda hapa katika uwanja wa mpira au nije katika shamba na kulichukua mahali hadi mahali kama tu Bwana atakavyoongoza. Na naona kwamba hivyo ndivyo Yeye atakavyotenda. Mnajua kuna ono kuhusu hilo. Na nafikiri kwamba labda hiyo sababu haya yanatokea . . . Sasa mwajua, mara nyigi tunafikiria ni vibaya sana kwa sababu mambo fulani hutokea, lakini mwajua, huyo huenda ikawa ni Mungu (mwaona?) akikusukuma katika mambo haya. Wakati Yeye alimenapo, atalitenda.

<sup>20</sup> Siku chache zilizopita wengi wenu—yapata mwezi mmoja kabla ya kwenda Afrika . . . Wengi wenu labda wana kanda (ninyi watu mnaopata kanda) juu ya *Kuchagua Bibi Arusi*. Ulihubiriwa California. Dakika chache za mwisho za kanda ile, sikumbuki kamwe kuhusu kuwepo huko. Lakini Roho wa Bwana alikuja kwa nguvu sana. Nalikuwa nikiwalaumia jinsi walivyokuwa wakiishi na kufanya, na baada ya Injili kuhubiriwa na kutangazwa mbele yao. Mara Roho Mtakatifu akanena na akasema, “Kapernamea (mwaona?), mji ule unaojiita wenywewe kwa jina la malaika (huo ni Los Angeles), wewe umejikuza mpaka Mbinguni, lakini utashushwa mpaka kuzimu!” Mnaona? Na kisha baada ya hayo ukaisha, naam, nilikuwa nije. Na Ndugu Mosley na Billy walikuwa pamoja nami, nao walisema . . . Walirudi wakaangalia, na sakafu yote ilikuwa imejaa watu, wahudumu wakilia kwa huzuni.

<sup>21</sup> Nami nalikwenda na kuchukua Andiko; nikasema, “Kuna kitu kuhusu hilo katika Biblia.” Na ilikuwa Yesu akikemea

Kapernaumu, miji yote ile ya pwani ambayo alikuwa ameizuru. Kwa nini alisema, "Nawe Kapernaumu, umetukuzwa mpaka mbinguni, utashushwa mpaka kuzimu." Alisema, "Kwa kuwa kama kazi zilizofanyika kwako zingefanyika katika Sodoma na Gomora, ingalikuweko hata leo." Na wakati ule Sodoma na Gomora ilikuwa chini ya Bahari. Na baada tu ya hilo, labda miaka mia moja au yo yote ile baada ya unabii wa Yesu, Kapernaumu, mji pekee wa pwani ambao yeye aliuzuru, tetemeko la nchi liliuzamisha baharini. Wajua, hilo ilikuwa jibu la moja kwa moja kwa California, kwa Los Angeles.

<sup>22</sup> Na kisha huko Tucson hivi majuzi, niliporudi tu, tetemeko kubwa la nchi lilitokea kule. Na wanasyansi walikuwa katika televisheni wakilichora. Ilikuwa katika magazeti, kwamba dunia hivi majuzi ilipasuliwa toka visiwa vya Aleusia—au toka Alaska kuzunguka Visiwa vya Aleutia, kama maili mia mbili kupenyeza baharini, ikurudi hadi San Diego, ikazunguka Los Angeles, na kutokea San Diego. Na iliachana inchi kadhaa. Nyumba zimebomolewa. Nyumba za kulala zimezama. Na mwanasyansi katika tume hii ati—aliulizwa, akasema, "Vema, hiyo yaweza kuanguka siku moja."

<sup>23</sup> Yeye alisema, "Ati yaweza? Itaanguka!" Naye alitumia majina ya kisayansi jinsi yale mawe ya volkeno yame... Hilo ndilo lilirosababisha haya matetemeko ya ardhi kuzunguka San Diego na chini ndani kule; imekuwa sehemu ile tupu. Na sasa yote imeanza kuporomoka kama changarawe inayobonyea. Na sasa ni ganda tu na imeachana inchi nydingi. Wangechukua rada na kadhalika na kufuatilia ufa ule, na kutia alama, kuona ilipokuwa. Na iliachana inchi nydingi zaidi, labda inchi mbili au tatu hivi majuzi, tena, mara tu baada ya kutolewa unabii ule.

Na wale waliokuwa wakimhoji mwana sayansi yule walisema, "Vema, labda jambo hilo halitatukia katika wakati wetu."

<sup>24</sup> Alisema, "Lingetukia katika dakika tano au miaka mitano, lakini patazama."

<sup>25</sup> Bibi Simpson—sidhani yuko nasi leo; au...ninamuona Ndugu Fred akiteti hapa, lakini sijui alipo Bibi Simpson. Alikwenda akapata unabii ambao niliutoa mnamo 1935 au kitu kama hicho, na kusema: "Wakati waja (imeandikwa katika kitabu mahali fulani) bahari itatiririka mpaka jangwani." Angalia litakalotokea. Kama hayo maelfu ya maili mraba yatakayotumbukia katika mawe ya volkano yanayoyeyuka ya dunia na kudidimia ndani, patakuwa na mamilioni watakaokufa kwa wakati mmoja. Na hilo litasababisha wimbi kubwa sana la bahari... Kumbuka, hadi kufikia Bahari ya Salten ni futi mia moja au mia mbili chini ya usawa wa bahari. Maji hayo labda yatakaribia sana Tucson na hilo wimbi kubwa la bahari likija huko. Na bahari itatiririka hadi jangwani.

Mataifa yanavunjika;  
 Israeli inaamka,  
 Ishara walizotabiri manabii;  
 Siku za mataifa zimehesabiwa,  
 Zimekubwa na hofu,  
 Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.

<sup>26</sup> Tuko wakati wa mwisho. Sasa, Bwana awabariki sana. Ninaanza hayo na kusahau saa. Tutafifia hivi karibuni katika umilele kwa vyo vyote.

<sup>27</sup> Na sasa, katika Marko Mt. sura ya 7 na aya ya 7, kuleta fungu la maneno kwenye somo hili ambalo ndio mara tu lisomwe katika 1 Mambo ya Nyakati 13. Ili kufanya somo kwa ajili ya hili nataka Marko 7:7:

...Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho  
*yaliyo maagizo ya wanadamu.*

<sup>28</sup> Sasa, sijui neno ila ule Ujumbe alionipa Bwana, na huo tu ndio niwezao kuzungumzia. Na sasa, nitazungumza juu ya somo asubuhi hii ambalo nilidhania lingefaa. Na usiku wa leo nataka kuzungumza juu ya, chakula kwa Wakati Wake, kama Bwana akipenda—*Chakula cha Kiroho kwa Wakati Wake, na Jinsi ya Kukipokea.* Sasa na asubuhi hii: *Kujaribu Kumtendea Mungu Kazi Bila ya Kuwa Mapenzi ya Mungu.*

<sup>29</sup> Mungu yu mwenye enzi. Na tunaona hapa Daudi alilofanya katika Maandiko yaliyosomwa ya 1 Mambo ya Nyakati 13. Naye alikuwa—makusudio yake yalikuwa mema. Lakini Mungu hatupi thawabu kwa ajili ya makusudio mema. Kuna njia moja pekee ya kumtumikia Mungu, nayo ni kwa kutenda mapenzi Yake kwa amri Yake. Naye Mungu, akiwa mwenye enzi, hakuna mtu wa kumwambia la kufanya au jinsi ya kulifanya; Yeye hutenda hilo namna... Anajua njia sahihi ya kilitenda. Na hilo hunifanya mimi njisikie vizuri. Na lapaswa kutufanya sisi sote kujisikia vizuri. Na nina hakika hutenda hivyo. Kwani mmoja atakuwa nalo likija namna *hii*, na mmoja atakuwa nalo likienda namna ile, na mmoja njia *nyingine*...

<sup>30</sup> Lakini kitu kimoja kikubwa tena kuhusu Mungu, Yeye hakutuacha, sasa, bila kujua ukweli ni nini na jinsi ya kuutekeleza. Hangelikuwa wa haki kutuadhibu kwa kutenda kitu ambacho hatukujua jinsi ya kikitenda, na kisha kutuachilia tujikwae katika kitu fulani. Si Mungu wa aina hiyo. Yeye ni Mungu ambaye hunena neno na anawatazamia wanawe kuliamini. Na kwa hiyo, Yeye ajua kilicho bora sana, na wakati wa kukifanya, na jinsi ya kukifanya. Sisi tunayo mawazo yetu juu yake, lakini Yeye anajua.

<sup>31</sup> Na kisha, kama Yeye angaliweka taratibu ya yale atakayotenda na hakutuambia yale yatakayotokea na jinsi yatakavyotokea, basi sisi tukijikwaa kwa hayo ingekuwa—tungehesabiwa haki katika—katika kujikwaa kwetu au kujaribu

kufanya kitu, kila mmoja angalihesabiwa haki. Lakini kuna njia moja pekee tu, nayo ni Neno lake.

<sup>32</sup> Na jambo lingine, Daudi hapa, twaona kwamba katika moyo wake alitaka kutenda jambo lililokuwa jema. Hakuwa na nia mbaya au hakuwa na kusudi baya, lakini nyumba—au sanduku la Bwana lilikuwa mbali na hao watu; naye alitaka kulirudisha sanduku la Mungu mahali pake, ili watu wamtake Mungu shauri kuhusu mambo waliyohitaji.

<sup>33</sup> Badala ya—ya kuliachilia tu, sisi... Vipi kama Ndugu Blair na baba wa mvulana huyu mdogo angesema, “Vema, ni vibaya mno kijana ameumia tu, ameuawa. Nadhani, kitu tu kilichotukia”? Lakini walimwendea Mungu haraka.

<sup>34</sup> Vipi kama maskini bibi yule, na mumewe ni mhudumu wa Injili, siku chache zilizopita usiku au siku, wakati bibi yule alipovunjikiwa na uti wa mgongo ambaye ndio mara asimame... Daktari alisema, “Atapooza maisha yake yote.” Vipi kama mumewe—bibi huyo alisema, “Vema, mpenzi, tutajifaraji tu kwa hilo.” Lakini haraka walifanya kitu kuhusu jambo hilo; walimwendea Mungu. Ni vitu vingapi katika Biblia tungeweza kuvitaja jinsi ambavyo watu wanapopata shida, humwendea Mungu.

<sup>35</sup> Vema basi, katika siku hizo walikuwa na mahali pamoja tu ambapo waliweza kukutana na Mungu, na hapo ni penye lile sanduku chini ya damu. Bado ndipo mahali pa kukutanikia, chini ya Damu. Kiti cha rehema kilinyunyiziwa kutoa neema kwa anayeabudu au anayeomba wakati alipomuomba Mungu haja yake. Naye Mungu alikuwa na utaratibu maalumu, njia iliyokupasa kuendea—kuhusu hilo, na Yeye asingalikubali kitu kingine cho chote. Asingekubali njia nyingine iliyotolewa, ni jinsi tu alivyoitengeneza.

<sup>36</sup> Hivi majuzi nimehubiri tu juu ya ujumbe (wengi wenu mwajua hilo) kwamba mna mahali pamoja tu palipoandalowiwa ambapo Mungu hukutana na mwabudu, mahali pale ambapo alisema, “Nitaliweka Jina langu.” Kama twaweza kupata kanisa ambamo aliweka Jina Lake, basi tumpapata mahali hapo. Alisema, “Sitawabariki katika malango yote, ni yale malango tu ambomo naliweka Jina Langu. Nitaliweka mahali pamoja nanyi yawapasa mkutane nami hapo; na hapo ndipo mahali pekee nitakapokutana nanyi.” Nasi tuliona kuititia hapo ambapo aliweka Jina Lake. Na hapo ndipo mahali pekee ambapo hukutana na mwabudu; na Jina Lake lilikuwa Yesu Kristo. Jina la Mungu ni Yesu Kristo.

<sup>37</sup> Yesu alisema, “Mimi nimekuja kwa Jina la Baba Yangu.” Kila mwana huja katika Jina la baba yake. Naye alikuja katika Jina la Baba. Na hakuna Jina jingine chini ya Mbingu lililotolewa mionganii mwa watu, au linaitwa Methodisti Presbiteria, Church of Christ, hata ifanyweje, kuna mahali

pamoja tu pa kukutania ambapo Mungu hukutana na mwanadamu, na hapo ni wakati awapo ndani ya Yesu Kristo, mahali pekee. Na mambo yote haya ya kale nyuma kule chini ya Agano la Kale ni kivuli cha hilo. Nawatakeni muelewe waziwazi hilo. Sasa, ni somo la shule ya Jumapili. Na nina baadhi ya Maandiko na maandishi yaliyoandikwa hapa. Nami niliwaza kwamba hili litasaidia muelewa, kwani mambo yote ya zamani yalitokea kama mifano kwetu sisi.

<sup>38</sup> Sasa, twaona kwamba Mungu alikuwa na njia ya kufanya mambo, lakini Daudi, akibarikiwa tu na Mungu kwa kuwa angekuwa mfalme, alifikiri tu kwamba angemtendea Mungu kitu kwa vyo vyote. Naye kamwe hakuliedea hilo kwa njia iliyokuwa sawa.

<sup>39</sup> Tunaona, Mungu hulifunua Neno Lake katika majira Yake Mwenyewe aliyoyachagua tangu awali. Sasa, Martin Luther angewezaje kujua kuhusu Ujumbe wa leo? Angewezaje Mpresbaiteria... Martin angewezaje—au kanisa Katoliki kujua ujumbe wa Martin Luther? John Wesley angewezaje kujua ujumbe wa Luther? Wesley angejuaje ujumbe wa Wapentekoste? Au Wapentekoste wangejuaje Ujumbe huu? Unaona? Yeye huufunua katika majira Yake, kwa sababu ni Mbegu; na kadiri ikuavyo na kukomaa hujifunua Mwenyewe.

<sup>40</sup> Kama joto la jua kuifungua. Inapokuwa nyororo na changa, kuichipusha toka ardhini, hiyo mbegu, kisha katika hatua nyingine ya jua kuipa majani yake. Jua kali litaiva kama ni mbegu ya kukomaa au wakati wa kukomaa. Kwa hiyo hulirekebisha jua na huyarekebisha maumbile kuafikiana na Neno Lake. Hulirekebisha Kanisa, waliochaguliwa tangu awali, Bibi-arusi, kukabiliana na majira wanayoishi.

<sup>41</sup> Hata maumbile yenye hantuambia leo, tunapoona mataifa yakivunjika, dunia ikididimia, maandiko kwenye ukuta. Tunaona kanisa na hali lilimo. Twamuona Bibi-arusi na hali aliyomo. Nasi twajua kwa mambo ya asili kwamba Kanisa linajiweka tayari kuondoka. Ni wakati wenye fahari vipi. Ni wakati ambao manabii wote walitamani kuuona, saa hii.

<sup>42</sup> Sasa, hulifunua Neno Lake katika majira Yake tu. Martin Luther alisoma Biblia ile ile tuliyosoma. Wesley alisoma Biblia ile ile Martin Luther aliyosoma. Wapentekoste walisoma Biblia ile ile tunayosoma. Yesu alisoma Biblia ile ile Mafarisayo waliyosoma, lakini walikuwa... Wakijaribu kuiweka ngano katika hatua ya mapema ambapo ilikuwa inaiva, walishindwa kuiona saa yao.

<sup>43</sup> Sasa Daudi amefanya jambo lile lile hapa. Mungu hulifunua Neno hili katika majira yake na kwa yule amchaguaye kulifunua kwake. Mungu huchagua wa kulifunua kwake. Alichagua hilo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Matendo Yake yote yalijulikana Kwake, yakiwa yamefichwa wanadamu; Yeye

huyafunua tu apendavyo. Ni majira Yake aliyochagua, mtu Wake aliymchagua. Na kamwe hajachagua kundi au dhehebu; ni mtu aliyechaguliwa. Jinsi atendavyo hilo.

<sup>44</sup> Ni nani yule atakayethubutu kumsahihisha na kusema, "Sasa, Bwana, ulifanya kosa kwa kumweka mtu huyu katika huduma. Mtu huyu haamini kama tuaminivyo." Nani atakayekwenda kumwambia Mungu amekosea katika jambo hilo? Itahitaji mtu ambaye ana hatia zaidi kidogo kuliko mimi kumwambia hilo. Yeye anajua atendalo. Anajua amchague nani na asimchague nani, la kufanya na wakati wa kulifanya. Haidhuru tunavyofikiri mtu fulani anastahili kufanya kazi fulani, Mungu anajua ni yupi anayestahili kwa wakati huo na majira hayo, au majira hayo na wakati unaofaa wa kuitenda.

<sup>45</sup> Naye Mkristo halisi na wa kweli, mwamini halisi na wa kweli katika Mungu, humngojea Bwana kwa mambo haya. Ngojea juu huduma yako. Kama ukijisikia kuitwa, hakikisha kwamba ni Mungu. Hakikisha kwamba ni sahihi. Hakikisha kwamba yale usemayo yako katika wakati. Biblia ilisema, "Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya. Watapanda juu kwa mbawa kama tai. Watapiga mbio, wala hawatachoka. Wakienda kwa miguu, hawatazimia."

<sup>46</sup> Angalia Daudi, mfalme wa Israeli; akiwa ndio tu apakwe mafuta. Samueli alimmiminia mafuta, naye alikuwa amechaguliwa na Mungu awe mfalme wa Israeli. Naye Daudi alipata ufunuo huu kulileta sanduku la Bwana hadi mji wa Daudi. Sasa, hakuna kosa lo lote, lakini unaona, Daudi aliliendea isivyo sahihi.

<sup>47</sup> Sasa, yaonekana kana kwamba mtu kama huyo angepata ufunuo, mtu mkuu kama mfalme aliyechaguliwa na Mungu (mfalme mkuu kuliko wote aliywahi kuishi duniani nje ya Kristo, nadhani, alikuwa Daudi, kwa sababu Kristo ni Mwana wa Daudi)... Sasa, mtu mkuu zaidi ya wote, aliyekuwa ndio tu apakwe mafuta, akitoka kwenye Uwepo wa Mungu hasa, alipata ufunuo kumfanyia Mungu kitu na alitaka kukifanya kwa ajili ya Mungu, lakini ule ufunuo ulikuwa sio sahihi. Sasa, hilo ni jambo kuu. Litahusu somo letu: *Kujaribu Kumfanyia Mungu Kazi Bila ya Kuitwa Kuifanya*.

<sup>48</sup> Angalia, Daudi alipata ufunuo. Na angalia, haikuwa nabii Nathanieli ambaye alipata ufunuo; ilikuwa mfalme Daudi ambaye alipata ufunuo. Wala Nathanieli hakutakwa shauri juu ya hilo. Hakumuuliza Nathanieli kamwe. Lakini uliona hapa katika 1 Mambo ya Nyakati, alifanya shauri na maakida wa maelfu na maakida wa mamia. Hakumtaka shauri Nathanieli kamwe. Aliwataka shauri watu, na aliwataka shauri pia makuhani na wanatheologia wa siku ile, waandishi na wanatheologia. Daudi kwanza alitaka shauri, kasema, "Hilo—kama hili ni la...Mungu, hebu basi tushuke twende huko

tukalete sanduku la agano la Mungu wetu mjini, na tumtake Mungu shauri kabla ya kufanya mambo.”

<sup>49</sup> Walisema katika siku za Sauli waliacha kumtaka shauri Mungu kwa lile—lile—lile sanduku, ile Urimu—Urimu Thumimu; waliacha kufanya hivyo. Kisha Daudi akasema, “Sasa, hebu na tururudie Mungu, sisi sote. Hebu na tururudie mambo yaliyo sahihi. Hebu tushuke twende huko tukachukue lile sanduku tuliletie hapa (tuulete Uwepo wa Mungu, kwa maneno mengine, mjini). Hebu tufanye ufufuo. Natuwarejeshe watu.” Lakini alipata ufunuo, ambao ilionekana kuwa mzuri, lakini hayakuwa mapenzi ya Mungu.

<sup>50</sup> Badala ya kuuliza chanzo ambacho alipaswa kuuliza, aliwataka shauri maakida wake, kwa sababu ndio mara tu awe mfalme, naye alifuatia mawazo kama hayo ambayo maakida wake na watu wake wakuu . . .

<sup>51</sup> Kisha akaenda katika kanisa la kawaida akauliza kama wangeweza kuwa na ufufuo: wale makuhani, waandishi, maakida wa maelfu, maakida wa mamia, naye akawataka shauri, “Je, hili lilikuwa mapenzi ya Bwana?” Nao wakasema ndivyo. Lakini, unaona, alishindwa kuuliza chanzo muhimu ambacho siku zote Mungu hutenda kazi kwake (unaona?); akashindwa kukipata.

<sup>52</sup> Sasa makusudio yake yalikuwa mema. Nia yake ilikuwa njema. Makusudio yake yalikuwa mema, na—kuleta ufufuo mjini, kuwarudisha watu kwa Mungu. Lakini kamwe hakutaka shauri jinsi Mungu alimwambia atende. Unaona?

<sup>53</sup> Hata watu wote walikubali na wale makuhani na—kwamba mfalme alikuwa sahihi. Walihitaji sanduku lirudi mjini. Sasa, walihitaji Uwepo wa Mungu. Walihitaji ufufuo. Lakini Mungu hakuwa ameahidi kufunua Neno Lake katika majira yake kwa watu. Hakuahidi kamwe kulifunua kwa mfalme katika majira. Naye Mungu habadiliki hata kidogo. Yeye hakuahidi kufanya hilo.

<sup>54</sup> Hata lifanywe kwa uaminifu vipi, na kwa nia nzuri vipi, na makusudi mazuri vipi, na hata watu wapende mambo hayo vipi, na kuona haja yake, kuna mapenzi ya Mungu yanayopaswa kutekelezwa katika mambo haya. Hilo ndilo ninalotaka kusisitiza sana usiku wa leo. Nataka kulifanya hili ili kwamba huna budi kuliona kama—kama Roho wa Mungu anakaa ndani yako. Na hiyo ndiyo sababu ninakawia sana hapa. Si kuchukua wakati wenu ninyi watu mnaosikiza kwa simu na kwenye redio za motokaa, lakini na—nawataka mulione hilo. Kama wakati wenu ukimalizika, chukueni kanda yake. Kwamba kuna . . .

<sup>55</sup> Haidhuru inahitajika vipi. Kila mmoja anakubali kwamba jambo hilo lahitajika, hata hilo liwe kweli vipi, bado kungali kuna kitu kimoja cha kutafuta: Je, hilo ni mapenzi ya Mungu?

Sasa, Mungu hakuahidi kamwe kwamba angefunua siri Zake kwa wafalme wake, angefunua siri zake kwa watu Wake.

<sup>56</sup> Kitu kama wakati wa Mikaya, mwana wa Imla. Kama tunapoliajcha, si fungu, lakini wakati mwingine, kulilingiza hili na kulifanya kweli kwenu, dhahiri kwenu, ili msilikose.

<sup>57</sup> Kulikuwako katika siku za Mikaya... Alikuwa mtu maskini, na pia alitoka kwenye familia maskini. Lakini Ahabu, mfalme wa Israeli, kama taifa likiwa chini ya Mungu, alitenga kando shule moja na alikuwa ameleta manabii walioeteuliwa, waliochaguliwa kwa uangalifu sana, naye alikuwa na mia nne wao chuoni. Nao walikuwa watu wakuu. Hawakuwa tu manabii wa uongo. Walikuwa manabii wa Kiebrania, watu halisi. Na walimtaka Bwana shauri kwa watu hawa. Nao walitabiri. Lakini unaona, wakati lile shindano halisi la kuamua lilopofika, kila mmoja alikuwa nje ya Neno la Mungu na mapenzi Yake.

<sup>58</sup> Kwani Yehoshafati alishuka toka Yerusalem kumlaki m—mfalme Ahabu, nao wakavaa mavazi yao, wakaketi langoni, na akawaleta manabii mbele yao. Kwanza Ahabu alisema, "Tunapo mahali hapa Ramothi iliyo Gileadi ambapo ni petu kweli." Sasa, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI: Yoshua aliwagawia watu na akawapa hapo, lakini Wafilisti walikuwa wamepachukua. Kisha kasema, "Hapa watoto wetu wanahitaji chakula, na hatuna ardhi ya kutosha kukuza chakula; na adui yetu, Mfilisti, huwalisha watoto wao, hao makafiri, katika ardhi ile ile ambayo Yehova Mungu alitupa sisi." Hilo ni dhahiri sana. Kisha kasema, "Hapa sisi, watu wa Mungu, tumeketi na watoto wetu wahitaji; na adui yetu analisha watoto wao katika ardhi ambayo Mungu alituitia toka Misri na akatupa sisi." Hilo lingemuinua Mthiologia, ama sivyo? Alisema, "Tutaenda tuchukue mashamba yetu ambayo Mungu alitupa?"

<sup>59</sup> Yehoshafati alisema, "Ndio, nitawasaidia. Sisi ni ndugu. Ninyi mko Yuda, na mimi niko katika—nimo Yerusalem" (au—au ilikuwa vinginevyo? Naamini... La, hilo ni sahihi, nafikiri kwamba Yehoshafati...) Hata hivyo, Yehoshafati alikuwa mtu mzuri, mfalme, mtu wa haki ambaye alimpenda Bwana. Ahabu alikuwa mwamini vuguvugu. Kwa hiyo waliwaleta, na Yehoshafati alisema, "Sikilizeni, na tumtake Bwana shauri kwanza. Yatupasa kujua hili." (Unaona, kama Daudi angalitenda kile Yehoshafati alitenda...) Alisema, "Tusitende hili?"

Na haraka, akiwa Mwisraeli, Ahabu alisema, "Bila shaka. Nina mia nne, Waebrania kama tulivyo sisi, manabii wa Kiebrania wa dhehebu letu. Na nitawataka shauri. Wao ni manabii."

<sup>60</sup> Sasa, waona, hili... Unasema, "Hilo hunikwanza, Ndugu Branham. Nabii?" Lo, ndiyo! Palikuwepo na mmoja katika wakati wa Yeremia ambaye alisema watakuweko huko miaka

miwili tu. Bwana alimwambia Yeremia, sabini. Akaweka nira katika shingo Lake, naye yule nabii Hanania akaivunja. Lakini Mnajua lilolompata. Lo, ndio! Yakubidi ukae na Neno.

Kwa hiyo manabii hawa walipanda, na wakatabiri, wakasema, "Kweeni, Bwana yu pamoja nanyi."

<sup>61</sup> Na mmoja wao, naamini ni—nasahau jina lake sasa, mkuu wao, Zedekia, naamini, alisema—aliweka pembe mbili za chuma akasema "Bwana asema hivi, kwa hili (sasa, mtu yule alikuwa mwaminifu) utawasukuma maadui zako warudi nyuma katika nchi zao na kuchukua kilicho cha Mungu; umepewa hiyo." Sihamini alikuwa mnafiki. Naamini alikuwa mtu mzuri. Naamini hao manabii wote walikuwa watu wazuri.

<sup>62</sup> Unasema, "Manabii?" Ndio! Kumbuka, mtu yule yule ambaye alikubali kumuua Yesu Kristo alitabiri, kwa sababu ilikuwa ni zamu yake. Alikuwa kuhani mkuu mwaka huo, na kwa kuwa hicho kilikuwa cheo chake naye alikishikilia hicho cheo, Roho wa Bwana alimjia. Na hilo halikumaanisha ameokolewa au cho chote kile. Na alitabiri (Kayafa) kwa sababu kilikuwa cheo chake kilichotenda hilo.

<sup>63</sup> Na hawa manabii, wakiwa manabii wa cheo cha manabii, walitabiri, na Roho wa Mungu aliwajia, watu walio na karama za Roho.

<sup>64</sup> Natambua ninazungumzia asilimia tisini na tisa ya Wapentekoste, lakini mtu... Mara nydingi mtu, Mungu anaweza kutenda kazi pamoja nao, awape kipawa, na watu watawabana watu hao. Kama hawakuwa wameitwa sawasawa na kutumwa na Mungu, atamfanya mwanamume huyo au mwanamke kusema kitu ambacho si mapenzi Yake, kwa sababu watu wanawashurutisha kulitenda.

<sup>65</sup> Jinsi ilivyonibidi kumshika maskini mchungaji wetu hapa juu ya jambo hilo. Nje huku mwituni asubuhi moja, mnamo saa 9 usiku, kasema "Nenda kamwambia Ndugu Neville!" Nilikuja kwako, sivyo, Ndugu Neville?

<sup>66</sup> Kila mtu, "Ndugu Neville, nitabirie. Niambie hili au lile." Unaona? Mtamfanya aseme mambo basi ambayo hayatatimia. Wao ambaeo hungojea kujua ambalo Bwana ataka kutenda. Waona?

<sup>67</sup> Kwa hiyo watu hawa waliliangalia katika hisi ya maumbile, "Ni yetu." Lakini waona, hawakutafuta Neno na mapenzi ya Mungu.

<sup>68</sup> Kisha Mikaya akashuka akaja, naye alikuwa na ono. Na akaangalia kwanza. Unatambua? Alisema "Ngoja. Nipeni usiku huu. Ngoja nitafute na kesho labda naweza kuwajibu." Hakuwa na haraka, "BWANA ASEMA HIVI," kama katika kupatana na manabii wengine; alisema, "Nitaseda tu asemayo Mungu." Na siku iliyofoata twaona Mungu alimwabia yatakayotendeka. Na

lilikuwa kinyume kabisa cha wale wengine. Chuo chote kilikuwa kinyume. Na hata mmoja wao aliondoka akaenda akampiga kofi la uso kwa ajili ya hilo. Lakini unaona, alingojea. Kisha alipofanya hilo alilinganisha unabii wake, ono lake, na Neno liliandoandikwa, na ulikuwa unapatana na Neno.

<sup>69</sup> Mtu asemapo wana ufunuo kubatiza watu katika Jina La Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, hilo ni kinyume cha Neno. Hamna mmoja kati ya hao wengine aliyewahi kutenda hivyo. Wakati wasemapo kwamba, “Lo, tutasimama...” na *hili, lile* na *lile lingine*, na kadhalika, hayo ni kinyume cha Neno. Wanaposema hawaamini katika uzao wa nyoka, hilo ni kinyume cha Neno. Na Mambo haya mengine yote, hilo ni kinyume cha Neno. Lazima ipatane na Neno na iwe katika majira yake.

<sup>70</sup> Sasa, laiti Daudi angefanya hilo. Sanduku lilikuwa lije, lakini si wakati ule. Hakukuweko na mahali pake.

<sup>71</sup> Angalia sasa, waliposhuka wakaenda kuchukua lile sanduku, hao mabwana wote walisema, “Hivyo ndivyo inapaswa kufanya, Daudi, Mungu atukuzwe! Twahitaji ufufuo.” Na hiyo ilikuwa Pentekoste halisi leo—Wabatisti, Presbiteria. “Daudi, wewe ni mfalme wetu. Ninji nyote... Akida fulani na Meya *fulani* na Jemadari *fulani* atakuwepo kwenye mkutano wako. Naam, wanasema hivyo ndivyo unapaswa kufanya, Daudi. Nchi yote iko pamoja nawe.” Hiyo ndiyo shida leo hii! Sitaki nchi. Nataka Mungu, kama hakuna mtu mwininge anayesimama.

<sup>72</sup> Daudi alikuwa na maakida wote. Alikuwa na ushirikiano na jeshi. Alikuwa na ushirikiano na madhehebu yote, na wathiologia wote, na wote—kila mtu akikubaliana naye. Hivyo ndivyo alivyofanya Ahabu, na wengine katika Maandiko; lakini hakuwa na Mungu, kwa sababu alikuwa nje ya mapenzi ya Mungu. Natumaini tunaelewa hili!

<sup>73</sup> Angalia! Walifanya kila kitu cha kidini walichoweza. Lazima labda waliweka matangazo na kila kitu: “Ufufuo mkuu, sanduku litarudishwa. Tutakuwa na ufufuo! Tutafanya *hili*.”

<sup>74</sup> Angalia, aliwatuma waimbaji. Aliwatuma watu wenye vinubi, walio na tarumbeta, na walitenda kila kitu cha kidini walichoju; na bado Mungu hakuwa katika hilo! Kwa namna fulani twalionia likijirudia tena, sivyo?

<sup>75</sup> Waliwachukua waimbaji wote. Walichukua wapiga vinubi wote, wapiga tarumbeta, wanawake wanaume, ye yote aliyeimba; wote waliwachukua chini huko, na walipitia kila kitendo cha kidini, sitaki kusema hili, lakini sina budi kulisema: Vivyo hivyo madhehebu haya leo hii, Wapentekoste na kadhalika, wanapitia kila kitendo cha kidini cha kuimba na kupaza sauti kwa nguvu.

<sup>76</sup> Angalia, Daudi alipaza sauti kwa nguvu zake zote, akapiga vigelegele akaruka, na akapitia kila tendo la kidini liwezalo

kuwepo; na bado Mungu hakuwa katika jambo hilo. Na nia yake, na makusudi yake, na kila kitu kilikuwa sahihi; lakini akapitia nalo njia isiyo sahihi. Unaona? Alifanya matendo yote ya kidini: alipaza sauti, aliimba, alikuwa na waimbaji maalumu, wapiga kelele maalumu, kila kitu. Walicheza katika roho. Walifanya kila kitu ambacho kilikuwa cha kidini.

<sup>77</sup> Ni kitu kama mikutano yetu mikuu ya wakati wetu. Walitaka kuushinda ulimwengu kwa ajili ya Kristo. Hakuna kitu kama hicho! Ufufuo mkuu wa halaiki ya watu, mambo makuu yakinoteka, laiti wangalitambua, siku hizo zimepita. Limeangamia! Lakini wanafanyiza mikutano mikuu, madhehebu na kila kitu; bali matokeo ni kama tu ilivyokuwa katika wakati wa Daudi; hayakufaa kitu.

<sup>78</sup> Twaenda na kuwa na ufufuo. Wajilisti—baadhi ya wainjilisti wetu wakuu leo, wanasema wana waongofu elfu thelathini katika muda wa majuma sita; na mwaka mmoja tokea hapo wakirudi, hawawezi kupata thelathini. Kuna kasoro fulani. Jambo ni kwamba, ni kitu kile kile tu alichofanya Daudi. Watu mashuhuri, mabwana, wahubiri wakuu, shule kuu, mamlaka makuu, lakini bado wangali wanataka shauri dhehebu la zamani badala ya kuangalia katika uso wa Neno la Mungu na kuona majira yataanza lini. Huwezi kukuza vyakula fulani ila nyakati fulani za mwaka.

<sup>79</sup> Sasa, na tuone nini kilichotokea. Ingawa—ingawa hangaiko lao la kidini na kadhalika lilikuwa kuu, makusudio yao yalikuwa makuu, mikutano ilikuwa mikuu, kuimba kwao kulikuwa kuzuri sana, kucheza kwao kulikuwa kuzuri sana, kupaza sauti kwao kulikuwa kukuu, mziki wao ulikuwa murua; na walikuwa na lile sanduku. Sanduku lina faida gani bila Mungu? Ni sanduku tu la mbao, meza mbili za mawe. Hivyo ni kama kufanya Ushirika, kubatizwa. Kuna faida gani kubatizwa kama kwanza hukutubu? Ina faida gani kupokea Ushirika na kuwa mnafiki, kama huishi maisha yale na kuamini Neno lile lingine la Mungu? Kuchukua Sehemu Yake na si lile lingine yaonyesha kuna kasoro.

<sup>80</sup> Sasa, wakati hili lote litokeapo...Na tuone sasa nini kinatokea wakati Mungu na kizazi chake, na wakati Wake, hafifikiriwi, ila tu mawazo ya watu.

<sup>81</sup> Watu wengi waniambia, “Kwa nini huji huku na kufanya mkutano? Vema, tunakuita. Tia sahihi *hili, lile* au *lingine*.” Ngojea! Mwaweza kutaka hilo, lakini je, Mungu anasema nini kuhusu jambo hilo? Watu wengi wameniambia...Nimekuwa na mwaliko, nimekuwa na mahojiano—mahojiano ya kibinafsii na kadhalika—nikangojea mwaka mzima. Ngojea! Nitajuaje la kusema mpaka Mungu aniambie la kusema? Mnaona? Yabidi kungoja. Hiyo ndiyo sababu nilisema, “Andika hilo, na hebu

nione alichosema.” Unaona? Ngoja. “Wao wamnganjeao Bwana watapata nguvu mpya.” Sivyo?

<sup>82</sup> Angalia, walimtaka tu shauri kuhani wa siku ile, na watheologia, madhehebu. Na tazama, kwa kufanya hilo, kumtaka shauri kuhani na kulitaka shauri kusanyiko, kuwataka shauri watu, walilitenda vibaya.

<sup>83</sup> Angalia! Sanduku lile lilikuwa Neno. Twajua hilo ni sahihi, kwa sababu sanduku lile ni Kristo, na Kristo ni Neno. Waona? Sanduku lile au Neno halikuwekwa kwanza katika mahali palipoamriwa, mahali pa asili palipoamriwa. Lo, msikose kuliona hili, Kanisa! Kila kitu kilikuwa kikamilifu, na kila kitu kilionekana kizuri, kama kwamba ufulufuo mkuu ulikuwa ukija; lakini kwa sababu walishindwa kumtaka shauri mtu yule aliyefaa kuhusu hilo... Waliwataka shauri kuhani, waliwataka shauri watu mashuhuri, waliwataka shauri watheologia, waliwataka shauri waimbaji na waliweka kila kitu mahali pamoja katika nia moja, na utaratibusi mkuu wa jeshi, na pia ma—ma—majeshi ya taifa, kila kitu kilikuwa kikichukuana na kingine kwa ajili ya mikutano mkuu; lakini walishindwa kumtaka shauri Mungu. Vivyo hivyo, Ahabu, hali kadhalika na wengine. Wakati wa jinsi gani.

<sup>84</sup> Sasa, usikose hili! Walishindwa kuipata, kwa sababu hawakutaka shauri. Na kwa kufanya hilo (angalia!), kwa kumwendea kuhani, kwa kuwaendea wale wanatheologia, na kwa kuyaendea majeshi, na kutokumfikiria hata mjumbe wao waliyepelkewa na Mungu wa saa ile, Nathani, walilifanya vibaya. Walikwenda na kulichukua lile sanduku na kuliweka juu ya gari jipyga, wakaliweka juu ya gari jipyga (au dhehebu jipyga litaanzishwa) na si katika njia iliyotolewa na Mungu, njia iliyochaguliwa kulichukua. Lilipaswa kubebwa kwa mabega ya Walawi. Lakini unaona, ukianza vibaya, utaendelea kukosea.

<sup>85</sup> Kama risasi inatakiwa ielekezwe kwenye shabaha, nawe usogeze ghafula mtutu vibaya hapa kiasi cha moja juu ya elfu moja kwanza, kwenye yadi mia moja umeenda kombo inchi nne au tano. Ulianza vibaya. Ee, Mungu tusaidie kujua kitu hiki kimeanza vibaya, mikutano hii mikuu ya wakati huu, kama inavyoitwa.

<sup>86</sup> Mungu hukutakwa shauri kuhusu hiyo. Makuhani na mtu wa kidini wanatakiwa shauri, madhehebu yalitakwa shauri. “Vema, mtakuwa na *hili na lile*? Naamini kama tungeweza kukusanya kila mtu pamoja...” Usiwakusanye watu pamoja! Chukua tu Neno la Mungu kuhusu hilo.

<sup>87</sup> Basi tunaona kwamba watendapo hilo, wanatenda nini? Huendelea mbele moja kwa moja na mipango yao ile ile ya kale ya kidini ambayo iko nje ya Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu. Kitu hicho kilikufa miaka mingi iliyopita, hayo mambo ya kale yaliyokauka ya miaka mingi iliyopita.

<sup>88</sup> Ilikwisha kauka katika siku za Bwana Yesu. Hawakujua hilo. Alisema, "Kama mngalimjua Musa, mngenijua Mimi, kwani Musa alisema nitakuja."

Walisema, "Baba zetu walikula mana jangwani."

<sup>89</sup> Alisema, "Wote wamekufa. Vipofu!" Aliwaita, Mafarisayo, viongozi wa dini. "Msiposadiki ya kuwa Mimi Ndiye, mtakufa katika dhambi zenu." Lakini hawakufanya hivyo. Walikuwa wameshika njia zao sana. Ilibidi wafanye watakavyo.

<sup>90</sup> Hivyo ndivyo Daudi alivyotenda hilo. Alilitenda alivyotaka, kwa hiyo alisema tu, "Unajua nitafanya nini? Tunaendelea." Alikuwa na ufunuo. "Tunaendelea sasa, kwa hiyo tutalifanya katika njia mpya. Siku za miujiza zimepit, kwa hiyo tutajitengenezea dhehebu jingine. Tutaunda gari jipy, na kuwaonyesha kitu kipyta kilichoanzishwa." Unabii wa uongo jinsi gani. Yakulazimu kurudia njia Mungu alivyosema litendwe.

<sup>91</sup> Waliliweka juu ya mabega ya Mlawi, na hiyo ilikuwa juu ya moyo. Sanduku lile, Neno, halipaswi libebwe juu ya dhehebu jipy, juu ya nadharia za mtu fulani, lakini moyoni. Neno la Mungu si la kushikwa-shikwa na madhehebu; lapaswa lishikwe na moyo wa mtu ambapo Mungu aweza kuingia mle ndani na kujifunua Mwenyewe. Na kama akilifunua kulingana na Neno, ni Mungu. Kama siyo, si Mungu. Halafu basi, Neno la majira hayo.

Hakika, Mfarisayo angesema, "Nani alituambia kwamba hatuwezi kufanya *hili* na kufanya *lile*? Musa alitupa amri hizi." Lakini Musa pia alisema . . .

Shetani alisema, "Naam, imeandikwa, atakuagiza . . ."

<sup>92</sup> "Na pia imeandikwa," alisema Yesu.

Majira yale, wakati ule. "Kama mngelimjua Musa . . . Mna mmoja awahukumuye, kama mngelimjua Musa, mngenijua Mimi," alisema, "kwani Musa aliandika habari Zangu: 'Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii mionganoni mwa ndugu zako; msikilizeni yeeye.' Kama wangalimjua Musa wangalimjua Yeye.

<sup>93</sup> Sasa sikiliza. Usikose hili sasa. Unaona, kitu cha kwanza walipomtaka shauri kuhani, walipowataka shauri watu mashuhuri, wakawataka shauri wanajeshi, wakawataka shauri kusanyiko lote, majirani kukusanyika pamoja kwa ajili ya mkutano huu mkuu ujao, walishindwa kufanya sahihi. Hawakumtaka shauri Mungu, na kwa kufanya hivyo, kutokurudi nyuma na kuona ilikuwa ni wakati gani . . .

<sup>94</sup> Ee ndugu, sikiliza! Twaishi wakati gani? Ni wakati gani? Tunaishi katika saa ipi? Si wakati wa mambo haya ambayo wanazungumzia. Hilo limepit. Hukumu inakaribia sasa. Unaweza kuiona ikianza. Unakumbuka mwamba ule uliokuwa juu ya mlima ule? Saa ya hukumu! Unakumbuka ule

ufunuo au ono la Bibi-arusi? Hebu aendelee kupiga hatua sahihi. Usimwache apige hatua baya.

<sup>95</sup> Angalia, katika mabega ya kuhanzi. Na Daudi na makuhani wote ambao hasa iliwapasa kujua vema zaidi, lakini ilikuwa nini? Makuhani walipaswa kujua vema zaidi. Waandishi, wanatheologia iliwabidi wajue vema zaidi, kwa sababu Neno lili sema wasifanye hivyo.

<sup>96</sup> Na leo wanapotaka kusema, “Loo, Yesu Kristo si yeze yule jana, leo, na hata milele; hilo ni kuwasiliana kwa mawazo; hilo ni *hili, lile au lile lingine*,” wanashindwa kuona lile Neno lililoahidiwa. “Loo, Hilo ilikuwa la siku iliyopita.”

Daudi alisema, “Loo, vema, sasa ngoja kidogo. Juu ya mabega ya—ya makuhani, hilo ilikuwa kule nyuma wakati Musa alipojitokeza. Hakika, sisi, tutaliweka juu ya gari jipya leo. Nina ufunuo wa hilo.”

Kuhanzi alisema, “Amina, Daudi.” Waona?

<sup>97</sup> Huku wameshawishiwa na hal mashauri mpya ya ekumenia kwamba iliwapasa waunganike na kufanya *hili hivi* na *vile*, hilo ndilo lililosababisha makuhani kujikwaa. Hawakumtaka shauri mtu anayefaa. Hawakulifanya sawa; kwa hivyo, waliingia matatani! Ndio!

<sup>98</sup> Nasikitika katika mambo mengi leo... Wakati mwalimu mkuu, mmoja wa Wapentekoste mashuhuri sana aliposimama mbele ya kundi la dini hivi majuzi usiku huko Chicago... Nalitarajiwa kuwa na mkutano ule pamoja na Wafanyi Biashara, lakini niliwaza nitakuwa Afrika wakati ule; lakini nilirudi tu siku moja kabla haujaanza. Nao walimchagua Mpentekoste maarufu aliyejaa bongo, naye alisimama akawaambia kwamba huu mwenendo wa ekumenia ulikuwa kitu cha Mungu. Na alisema wote wanarudi; hata kanisa Katoliki litarudia hali yake ya awali, wote wakinena kwa lugha kwa udhihirisho na kadhalika. Na bila kujua kwamba huo ni mtego wa ibilisi.

<sup>99</sup> Na mtu ambaye sikumjua... Wakati mw ingine unapanda mbegu. Haujui litakalotendeka. Lakini rais wa Wafanyi Biashara wa Injili Yote, mara tu msemaji yule mashuhuri alipoketi; akasema, “Kwa kawaida sisemi mambo dhidi ya wasemaji wetu, lakini hivyo sivyo Ndugu Branham alisema ingetendeka. Lakini alisema hilo litawaelekeza kwenye alama ya mynaya.”

Alisema, “Lakini Ndugu Branham hajui asemayo.” Akasema “Tuna—tunaamini anajua.”

<sup>100</sup> Na huko Chicago walisema ni wangapi hapa wangependa mimi kuja kutoa maoni yangu juu ya hilo. Walianza kulia kwa furaha na kupaza sauti. Unaona, unapanda mbegu. Hujui litakalotoke. Endelea tu kupanda Mbegu. Saa ile itakapowadia baadhi yake...

<sup>101</sup> Kama vile Thomas, alikuwa karibu mtu wa mwisho kumuona Bwana, lakini ilikuwa lazima amuone ili amuamini. Waona? Walipoliona likitokea, loo, Thomas akaingia, lakini alikuwa amechelewa kidogo.

<sup>102</sup> Sasa, watakapoona mambo haya ambayo yametabiriwa na kusemwa BWANA ASEMA HIVI yakitokea, basi watasema, "Tupeni mafuta yenu kidogo." Waona?

<sup>103</sup> Lakini sasa, angalia ushawishi. Wakati mwengine watu mashuhuri hukutanika pamoja. Unawasikia wakisema bwana mkubwa *Fulani* na bwana mkubwa *Fulani*, bwana wetu mkubwa...Usifanye hivyo kamwe. Hakuna watu wakubwa mionganii mwetu. Kuna mkubwa Mmoja tu, na huyo ni Mungu. Sisi ni ndugu na dada. Sijui kama u mchungaji wa kanisa ambalo lina watu watano, hilo halikufanyi mdogo; hilo hukufanya ndugu (unaona?), kama unalitii Neno la Mungu. Sijali nini, jinsi gani, huwi mdogo. Mungu hana watoto wadogo na watoto wakubwa. Ana watoto tu, na wote ni hali moja.

<sup>104</sup> Angalia, Mungu Mwenyewe alishuka akaja kutoka majumba ya kifalme yenye Utukufu ya pembe za ndovu kuwa mmoja wetu. Basi ni nani aliye mkuu? Alichukua...Hakushuka kuja hapa kuchukua namna ya kuhani, lakini mtumishi na kuosha udongo ule ule wa mfinyazi aliouumba, miguu ya wanafunzi Wake katika ile...Sasa ni nani aliye mkuu?

<sup>105</sup> Lakini walishawishiwa, watu hawa walishawishiwa. Hawakuelewa. Walifikiri kitu kipyä kitatokea (la), kitu ambacho Mungu hakusema kingetokea. Walikiendea kwa njia baya. Ndivyo ilivyo shauku yote hii wakati ile—ilipoanza nyuma kule miaka mingi iliyopita, kila dhehebu lilipaswa liwe na mponyaji wa Kiungu; kila dhehebu lilipaswa liwe na *hili*, *lile* au *lile lingine*. Kila dhehebu lilipaswa liwe na Daudi mdogo. Kila moja lilipaswa liwe na *hili*, *lile* au *lile lingine*. Unaona lililotokea? Ilifanya kitu kile kile ilifanya hapa. Kitu kile kile. Ushawishi...

<sup>106</sup> Neno kwa majira yake, waliupuuza wakati walimokuwa wakiishi.

<sup>107</sup> Angalia, mabega ya Walawi ndiyo njia ya awali ya Mungu aliyoandaa ya kufanya mambo haya. Beba sanduku hilo katika mabega ya Walawi. Kitu cho chote nje ya hilo kilikuwa kinyume. Alichosema, hicho ndicho alichomaanisha. Mungu hawezi kubadilika. Hiyo ndiyo sababu ya kukaa na Neno Lake.

<sup>108</sup> Nina 1 Mambo ya Nyakati 15:15, kama unataka kuandika hilo. Angalia, sasa angalia, hapo katika kumfuata Mungu... Sasa, nataka wewe u—upate kuandika hili bongoni mwako. Kushika amri za Mungu, kufanya kitu cho chote sawa sawa kwa Mungu, kufanya—kumfanya kazi kwa usahihi, kuna lazima tano, kumfanya Mungu kazi kwa usahihi.

<sup>109</sup> Sasa, Daudi alikuwa akimfanya Mungu kazi. Alikuwa akifanya kila kitu alichojuwa kufanya, isipokuwa kumuacha Mungu. Unaona? Alikuwa akifanya kitu ambacho kilikuwa sahihi, kitu kizuri kwa watu, kitu kizuri kwa kanisa.

<sup>110</sup> Lakini kuna lazima tano; nawatakeni mkumbuke haya. Haidhuru mtu ni mwaminifu jinsi gani katika kufanya jambo, kumtendea Mungu kazi, hili—hizi tano lazima ziwepo:

Kwanza, lazima iwe ni wakati Wake wa kuitenda.

<sup>111</sup> Vipi kama—kama Musa angekuja kasema, “Tutakuja kujenga safina na kuieleza juu ya Nile kama Nuhu alivyofanya?” Wakati wa Nuhu ulikuwa sawa kwa safina, lakini si wakati wake.

<sup>112</sup> Vipi kama Yesu angekuja, kasema, “Sasa nitawaambia tutafanya nini. Tutapanda juu mlimani kama Musa alivyofanya na kupata tangazo jipy la sheria? Unaona? A, a! Yeye alikuwa sheria ile. Unaona? Lazima wewe uwe katika wakati Wake. Lazima iwe katika majira Yake. Umelipata hilo sasa?

<sup>113</sup> Sharti iwe katika wakati Wake Yeye. Lazima iwe katika majira Yake, wakati na majira, na lazima iwe kulingana na Neno Lake ambalo limenenwa. Lazima . . .

<sup>114</sup> Sijali unasema vema jinsi gani *hili* lapaswa kutokea, ama *hili* lapaswa kutokea, au *hili* lapaswa kutokea, lazima liwe lalingana na Neno Lake, kulingana na wakati Wake na majira yake; na ni lazima litolewe kulingana na mtu yule aliyemchagua kulitenda.

<sup>115</sup> Sijali watu ni wakuu vipi. Hapo pana mfalme Daudi mkuu kama ye yote wao. Alikuwa mfalme juu ya taifa lile. Lakini Yeye alikuwa na njia ya kulifanya, naye alikwisha waambia jinsi ambavyo angalitenda. Lakini walishindwa kulifanya.

<sup>116</sup> Lazima iwe ni kulingana na Neno Lake, kulingana na wakati Wake, kulingana na—mpango Wake; na sharti ifanywe na mtu yule aliyemchagua kulitoa na kulifanya.

<sup>117</sup> Musa alijaribu kuikimbia. “Chukua mtu mwingine!” Lakini Mungu alimchagua Musa kuifanya. Wengi wao . . . Paulo alijaribu kuiipa, wengine wengi. Lakini lazima ifanywe na mtu yule amchaguaye kulitenda. Na lazima lije kwanza kwa manabii Wake. Neno la Mungu, halina budi kuwajilia manabii Wake, Amosi 3:7. “Bwana Mungu hatafanya neno lo lote mpaka kwanza alifunue kwa mtumishi wake nabii.” Nne.

<sup>118</sup> Naye nabii lazima athibitishwe na Neno la Mungu.

<sup>119</sup> Lazima zako tano ndizo hizo. Lazima iwe hivyo; wakati Wake; majira Yake (wakati aliposema itakuwa); na mtu yule aliyemchagua, na lazima ije kwa nabii; na nabii yule lazima awe nabii aliyethibitishwa. Tunaona wengi wao katika Biblia iliwajilia manabii nao hawakuthibitishwa. Nabii wetu ni Yesu Kristo.

<sup>120</sup> Kwa hiyo sasa angalia. Unaona, Mungu hakuwa amefunua kitu kile kwao kwa njia Yake aliyoandaa ya kukifanya. Walikubali njia ya Daudi. Walikuwa wamekubali njia ya kuhani. Walikuwa wamekubali njia ya waandishi, ya wanatheologia, lakini si njia ya Mungu. Nathanieli alikuwa—alikuwa nabii wa siku ile. Baadaye Nathanieli aliwaambia jinsi ya kulifanya. Lakini waona walilitenda bila ya kumtaka shauri Nathanieli. Hakuna neno lisemalo kwamba Nathanieli alitakwa shauri. Ushawishi wote ule, jambo lile kuu likiendelea...Na, jamani, naufikiria wimbo ule;

Hebu—niweke, nisaidie Bwana miyo  
inapowaka moto,  
Niache niyadhilishe majivuno (niende pamoja  
na wengine wao) na kuliita tu Jina Lako;  
Nifundishe kutotegemea yale wafanyakayo  
wengine,  
Lakini ningojee tu katika maombi jibu toka  
Kwako.

Hivyo ndivyo ilivyo. Hebu nione likitokea katika njia sahihi, kisha linaaminiwa.

<sup>121</sup> Sasa, Mungu alifunua jambo lile kwao kwa Daudi, na kwa wahudumu, na kwa watu, na kwa maakida wa maelfu, na maakida wa mamia, lakini sio kwa Nathanieli ambaye alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Na Bwana alisema asingefanya lo lote mpaka amuonyeshe kwanza nabii yule wa wakati ule la kufanya. Unaona walilotenda? Walitoka moja kwa moja katika Neno la Mungu, walikwenda wakaliweka sanduku katika gari jipya. Unaona? Kwa hivyo walikwenda kulisenda mbali na amri ya njia ya Mungu aliyoandaa...Na hilo ndilo limetokea leo, marafiki. Hiyo ndiyo sababu tumekuwa na mikutano mikubwa sana na kadhalika na bila matokeo. Kumkana Mungu zaidi, dhambi zaidi...Nakuambia, taifa hili limekwisha, si taifa hili tu, lakini mataifa mengine. Taifa hili kama Uingereza ya wakati mwingine limekuwa kahaba wa mataifa mengine yote.

<sup>122</sup> Kule mbali katika Mozambiki, maili mia nne na themanini toka kweni ustaarabu, msituni, watoto walioharibikiwa na akili wanamsikiliza Elvis Presley, wakitikisa vichwa vyao na kurukaruka juu na chini hivyo wakikaa usiku kucha na kukaa—na redio dogo kama hivyo wanazilinganisha maelfu ya maili mpaka Rhodesia kupata Elvis Presley. Na bado wanasesma, “Ni mtu wa kidini sana, yeye, na Pat Boone na wengine.” Naam, ni Yuda wa wakati huu, na hawajui hilo. Na hiyo ndio sehemu baya. Wanaamini wako—wako sahihi. Yesu hakusema kwa Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, “Wewe u uchi, na mwenye mashaka, na mnyonge, na kipofu, nawe hujui?” Hujui hilo!

<sup>123</sup> Vema, watoto wa Kipentekoste huko Afrika na mahali pengine wanasesma, “Vema, Elvis Presley, hujawahi kusikia

kuimba kuzuri kama Kwake.” Hakuna shaka Daudi alifanya hilo pia; hakuna shaka waimbaji walifanya hilo, lakini lilisababisha kifo kuipiga kambi. Mnaona walipo—tulipo leo marafiki?

<sup>124</sup> Mabega ya Walawi ilikuwa njia ya asili ya Mungu kufanya hilo, na walikuwa wameliweka juu ya gari jipya. Sasa, haitafanya kazi. Hawakutaka shauri ipasavyo. Unaona? Kwa hiyo walitoka kwa ajili yake na kuliendea kwa njia iliyo makosa, na hivyo ndivyo imetendeka leo.

<sup>125</sup> Wakati watu, haidhuru u mwaminifu jinsi gani, wanapojaribu kumfanyia kazi Yeye nje ya njia yake aliyoandaa ya kufunua, siku zote wanaivuruga. Mungu huliweka katika njia Yake. Mwanadamu, haidhuru u mwaminifu jinsi gani kujaribu kulifanya nje ya hiyo, u—utalivuruga.

<sup>126</sup> Kitu kama Baalamu alivyokuwa katika siku za Baalamu. Mungu alimwambia Baalamu, nabii yule... Alikuwa nabii, nabii Baalamu. Alikuwa nabii, na lile Neno lilimjia sawa kabissa, kasema, “Usiende huko. Hao ni wateule Wangu; hao ni chaguo Langu.”

Kisha Baalamu aliambatana na watu mashuhuri, na wanajeshi, wahubiri, watu walioshawishiwa, na akasema, “Vema, na—nawaambieni, mfalme ata...” Unaona, inafanana na Daudi, inafanana na siku hizi, chukua kila kitu tu kwa mfano, na utalionia. Ukiliona sema, “Amina!” [Kusanyika linasema, “Amina!”—Mh.] Unaona, unaona? Kama tu ilivyo sasa.

<sup>127</sup> Lakini wale—wale—wale makasisi walisema, wale—wale—wale—wale—wale makuhani walisema, waandishi walisema, wanatheologia walisema, “Hivi ndivyo inavyopaswa kutendwa.” Lakini haikuwa hivyo! Na ilidhihirisha haikuwa hivyo.

<sup>128</sup> Kisha Mungu akamwambia Baalamu—kwa maana alikuwa nabii kwanza—alimwambia, “Usiende huko!”

<sup>129</sup> Lakini ushawishi wa hawa watu wengine ulimfanya kulifanya kinyume cha vile Mungu alisema lifanywe, halafu ilikuwa laana badala ya ufufuo. Loo, hakika, alishuka akaenda kule akawafundisha watu, akisema, “Sasa tazama! Ngoja! Mwajua nini?” Kasema; “Sisi ni—sisi ni Wamoabu. Mnakumbuka, binti wa Lutu ni malkia wetu. Ndiye chanzo chetu. Wote tu wa damu moja. Wote tu... Sisi madhehebu yote ni kitu kile kile.” Usichanganyikane na kitu hicho. Usikikaribie. Unaona? Kwa hiyo alisema, “Sote tu kitu kile kile. Naam, watu wenu ni kama watu wangu. Twaweza kuoana mionganoni mwetu, tupate kuwa na halmashauri ya ekumeni hasa. Unaona? Sisi sote twaweza kukusanyika na kurudia kile kitu cha asili tena.” Na Mungu akalaani kitu kile. Dhambi ile kamwe haikusamehewa Israeli. Ilikaa nao siku zao zilizobakia. Na haikusamehewa kamwe. Waliangamia jangwani nayo (hiyo ni kweli!), kwa kuwa hawakuchukua njia iliyoandalika na Mungu kwa njia Yake iliyodhihirishwa ya kulifanya.

<sup>130</sup> Angalia, kitu hiki ambacho walifanya kilisababisha Israeli kufa kifo huko jangwani, na Yesu alisema, “Kila mmoja wao ameangamia na kutoweka.” Angalia ni nani aliyesimama na Musa nyuma kule Yoshua na Kalebu na ule—na ule mpango.

<sup>131</sup> Angalia tena, hapa pana Daudi, alichotenda. Na alipofanya hivyo, nini ilitendeka? Ilisababisha kifo kimpige mtu mwaminifu. Na nadhani bado tumeunganishwa kwa radio, nami nawatakeni ninyi msikie nchini kote. Kitu hiki Daudi alichofanya bila ya kumtaka shauri Nathanieli na kupata Neno la Bwana kwa ajili ya hilo, kilisababisha kifo kiwapige watu waaminifu. Naam, hapo aliunyosha mkono wake, ambao ulikuwa ukikaa kwenye uwepo wa lile sanduku, ultoka kwenye—kwenye nyumba yake. Na maksai akakunguwaa, na sanduku likianguwa likianguwa.

<sup>132</sup> Walikuwa wamekwisha tenda kitu kimoja kisicho sahihi, mambo mawili yasiyo sahihi. Kwanza, hawakuntaka shauri Nathanieli. Jambo jingine walilofanya walikwenda huko bila kuliangalia Neno la Mungu ambalo lile—Samuel alikuwa Neno katika siku ile. Nao kamwe hawakuliangalia Neno la Bwana, basi walipotenda, walikwenda kinyume na Neno la Mungu. Na hapa mtu huyu mzuri, ambaye alikuwa muangalizi—alikuwa askofu—alifikiria, “Vema hapa, sitaki Mungu aaibishwe.” Kwa hiyo akaweka mkono wake juu ya sanduku, ambapo yeye hakuwa Mlawi, naye akafa—mambo matatu.

<sup>133</sup> Sasa fikiria sana na tazama ambacho madhehebu wamefanya leo. Unaona? Wamelikataa, wameliita mafundisho ya uongo. Unaona? Angalia walipo. Watakuwa na halmashauri yao ya ekumeni haidhuru. Wameliita uwezo wa kuitishiana mawazo kiakili. Wakati Mungu Mwenyewe analithibitisha kuwa Ukweli na kuhakikisha ni Kweli. “Loo, wao ni kikundi kidogo tu cha watu wasio na akili kule,” wao husema; “hawajui wanachonena.” Hilo ni sahihi; hatujui. Lakini twanena maneno Yake tu, naye anajua analosema. Unaona? Siwezi kuelezea hilo, hakuna anayeweza, lakini Yeye—Yeye hulidhibitisha.

<sup>134</sup> Sasa angalia. Mara nyingi mwaminio wa kweli ajaye kwa Kristo, anataka kuja kwa moyo wake wote, huuawa kiroho namna ile ile. Watu wengi waaminifu huenda kwenye kanisa Katoliki wakitaka wawe Wakristo, huenda kwa Wamethodisti, Wabatisti, Church of Christ, na hata Wapentekoste (unaona), na wanataka kuwa Wakristo, anaweka mkono wake juu yake, anajunga nao.

<sup>135</sup> Naye Daudi alipoona jambo hili likitokea, lilimwamsha. Usiamke huku umechelewa sana huko, ndugu. Aliona kwamba mauti yamewapiga. Nionyeshe matokeo. Kwa nini huu uitwao ufufuo kuwarudisha makanisani umefanya katika taifa kwa wale—kwa kundi la waamini? Si kitu ila umetengeneza taratibu

mpya na madhehehebu wakati huu wote, wanachama zaidi na kadhalika. Taifa limekuwa na hali nzuri zaidi?

<sup>136</sup> Walisema walikuwa wakienda... Marekani—“Mungu aibariki Marekani, ni—ni taifa, ni nchi ya Kikristo.” Iko umbali wa maili milioni moja kutoka kwa nchi ya Kikristo! Wala hata siiombei. Nawezaje kuiombea, nayo haitatubu chini ya nguvu kuu za Mungu zilizoonyeshwa mbele yake, na kukana, na kufungia milango na kuzipa kisogo? Naikabidhi kwa Mungu. Na linaenda mbali zaidi, na sasa litazama. Tazama tu yatakayotendeka.

<sup>137</sup> Watu wengi waaminifu huenda kujiunga na dhehebu au kundi fulani au kikundi kilicho jitenga cha namna fulani, na hapo hufa kiroho. Huwezi kuwaambia kitu. Wanashindiliwa takataka hizo: “Naam, maaskofu hawa walisema *hili*, na *huyu* alisema *hili*; *huyu* alisema *hili*.” Unawaonyesha papa hapa katika Neno la Mungu ambapo ni BWANA ASEMA HIVI, “Lakini mchungaji wetu...” Sijali mchungaji wenu anasema nini, sijali nisemalo, au mtu mwagine asemalo. Kama ni kinyume cha Neno la Mungu lillothibitishwa, la saa hiyo, wakati huo, Ujumbe ule, na kadhalika, lisahau! Kaa mbali nalo. Na yanipasa nisimame mbele ya kila mmoja wenu katika siku ya hukumu, nanyi mwajua hilo. Na singethubutu kusema hilo, nikijua mimi ni mzee sasa. Nita... Si kwamba najua kitu, lakini Yeye anajua. Nafuata tu yale aliyo sema.

<sup>138</sup> Angalia leo ile mikutano mikubwa tume kuwa nayo nchini mwote, imethibitisha kwamba imekuwa bure. Na je, Yesu hakusema hapa sasa, Luka 7:7, “Nao waniabudu bure. (Daudi alilipandisha sanduku bure, Ahabu aliwafunza hao manabii bure. Baalamu alichukua fedha ile bure!) wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu”? Maagizo ya Mungu ndiyo jambo muhimu. Haidhuru jinsi gani...

<sup>139</sup> “Hao watu ni waaminifu kwelikweli.” Unasikia hilo sana. “Ni waaminifu sana.” Vema, hilo halimaanishi kitu. Shahidi wa Yehova, Seventh Day Adventist, na vikundi hivyo vyote vilivyo jitenga wanakuja barabarani hapa na kutenda mambo ambayo mmoja wetu asingalitenda. Wakatoliki wanasi mama pembeni na kuomba na kadhalika, na vyama hivyo vyake, vyenye mabilioni mara bilioni mara bilioni ya dola, bado wanaziomba. Waaminifu, bila shaka. Makanisa yanakwenda na—na kuhubiri na kadhalika, na wahudumu wanasi mama mimbarani na kufanya kila kitu wanachoweza kufanya kuingiza wanachama wapya katika kanisa lao; lakini ni sanduku jipyta. Kuna Sanduku moja tu la kufuata; hilo ni Neno la Mungu. Kitu cho chote dhidi ya Sanduku hiyo, kaa mbali nacho; kiko juu ya gari jipyta na si katika mabega ya Mungu. Hilo ni sawa. Kaa mbali na kitu kile. Usijishughulishe nacho kamwe.

<sup>140</sup> Mikutano yetu mikubwa, mabilioni na mamilioni wameungama. Nami nashangaa kama kutakuwepo mia moja wao toka kwa hiyo yote. Unaona? Haimaanishi kitu. Kisha angalia ahadi ya Neno.

<sup>141</sup> Utafikiria kwamba hiyo imeshindwa, na tunajua imeshindwa. Baadhi ya wa—wanaufufuo wetu mashuhuri sana nchini leo husema kwamba hiyo imeshindwa kabisa. Kanisa linajua imeshindwa. Kila mtu anajua imeshindwa. Vema, ni kwa nini? Kwa nini ikashindwa? Ni kwa ajili ya kusudi jema; ilikuwa ilete watu kwenye uwepo wa Mungu, mikutano mikuu. Na mamilioni ya watu wametumia fedha zao na kuziweka katika mikutano mikuu, na makanisa yote yakaungana pamoja, majumba makubwa ya mikutano, na mambo makuu, na mambo makuu yaliyofanyika; Kwa nini imeshindwa? Ilikuwa kwa sababu hawakujua kamwe saa ile waliyokuwa wanaishi. Si ajabu Yesu alisimama, na katika moyo Wake akalia; machozi yakimtiririkia mashavuni Mwake, naye alisema, “Yerusalem, Ee Yerusalem, mara ngapi nimetaka kuwakusanya kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake. Umempiga mawe kila nabii niliyempeleka kwako. Lakini hukutaka. Lakini sasa saa yako imefika.”

<sup>142</sup> Je, huwezi kuhisi Roho Mtakatifu akilia akitoka ndani yako? “Ee, Marekani na ulimwengu, mara ngapi ningewakusanya, lakini hamkutaka. Sasa, saa yako imekuja. Mungu wenu wa anasa, Mungu wenu wa uchafu, mungu wako wa Sodoma na Gomora, ambaye amekuja mionganoni mwenu...” Hata watoto wetu, wadogo, walio na nyewe zilizonyolewa kama za beatle na kukatwa kukingama nyuso zao, mambo madogomadogo ya kupotosha yakianza. Wanawake wetu wamekwisha! Hawakomboleki. Wanaume wetu wamekuwa majike wakubwa, wakienda wamevaa kaptura wakijifanya kama msichana, na nyewe zikining’inia shingoni, na... Tumekuwa Walawiti, na moto na hasira ya Mungu watungojea.

<sup>143</sup> Unajua jinsi atakavyoua, jinsi atakavyouharibu? Jinsi afanyavyo siku zote. Kahaba alipotenda kitu cho chote kisicho sahihi, aliuwawa kwa kupigwa mawe. Waliokota mawe kumuua mwanamke aliyekuwa kahaba. Hivyo ndivyo atakavyoliwa kanisa. Biblia ilisema atanyesha mvua ya mawe toka mbinguni, yatakuwa na uzito wa ratili mia moja kila moja, naye atawapiga kwa mawe. Nani atamzuia? Sayansi gani itakayosema haiwezekani? Atalifanya vile vile alivyotengeneza safina na akamweleza Nuhu kwenye usalamu; atafanya hilo tena kwa Kanisa Lake. Na kwa sheria Zake, na kwa njia Yake, atampiga kwa mawe kahaba yule ambaye ametenda uzinzi na wafalme na maakida wa mamia na maelfu. Atamuua kwa kumpiga mawe kwa sheria Zake mwenywewe ambazo ameweka katika utaratibu. Nani atamwambia Yeye hawezi kutengeneza mvua ya mawe?

<sup>144</sup> Uliza mtu ajuaye jinsi tone la mvua linavyoanza, na duara na kurudi katika . . . ? . . . na kukusanya zaidi na zaidi na zaidi hadi linafikia uzito fulani, kisha linaanguka. Yeye, ni Mungu ambaye nguvu za uvutano hata hazikuweza kumshikilia duniani na akainuliwa Mbinguni, Mungu, ambaye alitengeneza nguvu ya uvutano, pia anaweza kutengeneza . . . ? . . . kubwa vya kutosha kuning'iniza jiwe mpaka liwe na uzito wa ratili mia. Alisema atafanya hivyo, na atalifanya. Nani atamwambia asilifanye? Atalifanya kwa sababu alisema angelitenda.

<sup>145</sup> Tuko katika siku za mwisho. Tunasimama karibu na hukumu. Kwa sababu gani? Wanajaribu kula mana ya kale ambayo ilianguka nyuma kule miaka hamsini iliyopita, kanisa la Kipentekoste. Kanisa la Holiness linajaribu ku—zaidi ya miaka mia mbili iliyopita, Waluteri kama miaka mia tatu au zaidi iliyopita, mamia ya miaka iliyopita. Wanajaribu kula mana ya kale, Ee, ndugu, kitu hicho kimeharibika. Kimechafuka. Kita . . . Kina—Kina—siku zote nimesema —wadudu ndani yake, mabuu. Kitakuuwa ukila.

<sup>146</sup> Chunguza kama Daudi au kama ye yote wa wale wengine laiti angetaka shauri toka kwa Mkate wa saa hiyo. Laiti makuhani, na manabii, na wahubiri, na wanatheologia, na vyuo, na madhehebu wangeangalia ule wakati, lakini sasa haitawafaa kitu. Umekwisha sogea. Haitasaidia hata, chembe. Limekwisha sasa. Limevuka mstari huo kama miaka mitano iliyopita, kati ya toba, hukumu, na rehema.

<sup>147</sup> Angalia, kuna nini sasa? Ifanyweje? Tutafanya nini? Hebu tumtake shauri nabii, Biblia, ambapo hatuwezi kuongeza au kupunguza. Kama tukifanya hivyo, Mungu atatuondoa katika Kitabu cha Uzima. Biblia ilisema katika Malaki 4 jambo gani lingeteneka leo, Ufunuo 10, jinsi zile Muhuri Saba zingefunuliwa na kufunua siri hizi zote ambazo zilikuwa zimefichwa katika hawa watengenezaji. Alisema jinsi litakavyotendeka. Limo katika Biblia, BWANA ASEMA HIVI. Mungu amethibitisha hilo kabisa na kwa ukamilifu na kulihakikisha kuwa Kweli kwa ishara, maajabu mbinguni na angani, na kila kitu kingine kwa miaka thelathini na mitatu. Unafikiri watalisikiliza? La, wamekuwa. Wameuweka mkono wao juu ya jambo ambalo limeua kitu hicho chote. La, haiwezekani—haiwezekani, kamwe tena.

<sup>148</sup> Ilikuwa wakati kitu hiki kilipotokea ndipo Daudi akaona. Ee, Mungu, tupelekee Daudi ambaye anaweza kuona anaposimama, ambaye aweza kuangalia na kuona Mungu alifanya ahadi ambayo—jinsi angetenda leo. Mungu amelinena papa hapa katika Neno Lake jinsi angelitenda.

<sup>149</sup> Mungu alimwambia Mikaya; Mikaya alichunguza ono lake mbele ya manabii mia nne mashuhuri. Alichunguza ono lake, kuona kama kwamba ni sahihi. Aliangalia kule nyuma kwa yale nabii aliyemtangulia alisema kuona kilichotokea. Alitazama

nyuma, naye akaona kwamba Eliya aliposimama pale, alisema, “Ahabu, mbwa wataramba damu yako pia.” Sasa, aliona basi kwamba ono lile lililingana kabisa na Neno la Mungu, kwa hivyo akalitamka; naye alikuwa sahihi. Hilo ni sawa. Haidhuru wengine wao walisema nini, alidumu na Neno lile.

<sup>150</sup> Sasa, hebu na tuangalie lile ono tulilo nalo leo hii. Je, ni kujenga makanisa? Ni kujenga vitu vipyta? Ni mambo makubwa yatakayotendeka, au ni hukumu? Tazama nyuma uone ahadi ya leo. Ona majira tunayoishi.

<sup>151</sup> Wasema, “Mungu na abarikiwe, ndugu, mimi ni mwaminifu. Naijunga na kanisa. Nina shahada yangu ya sanaa. Nimefanya *hili*.” Hivyo ni sawa. Hivyo ni vyema; silipindi kamwe. Daudi alikuwa nayo pia; na makuhani wa siku zile pia, na wanatheologia pia; lakini ilikuwa dhidi ya Neno.

<sup>152</sup> Mungu alisema jinsi atalitenda leo, jinsi angerudisha mambo yote, lile ambalo angetenda tena. Aliahidi kurudisha. Hilo ni kweli kabisa. Katika Yoeli 2:28 aliahidi kurudisha: “Nitawarudishieni, asema Bwana, hiyo miaka iliyoliwa na parare.” Wana... Waona, huyo ni mdudu yule yule. Yuko katika hatua tofauti ya uhai. Na Ukatoliki ulipoanza kula, kisha Ulutheri, Wamethodisti na Wapentekoste na wote, chini, alisema, “Nitarudisha kila kitu Kanisani vile vile hasa lile lilitiyokuwa hapo awali.”

<sup>153</sup> Tazama ono lile hivi majuzi. Bibi-arusi yule yule hasa aliyejuka upande *huu* ndiye aliyejuka upande *huu*. Baada ya kahaba yule kupita wamevaa majoho yao, vitu vyao vidogovidogo vya kale vikiwa tu upande *huu*, na wakicheza rumba na wakijiita kanisa. Wasema, “Vema, sisi hatufanyi hilo.” Hivyo ndivyo Mungu anavyowaona. Si vile unavyojiona wewe mwenyewe; ni vile Mungu akuonavyo. Hakuna mtu anayejiona mwenyewe anakosea. Ni wakati unapotazama katika kioo cha Neno la Mungu, linakuambia kama unakosea au la. Kama Daudi angalitenda hilo, angaliona alikuwa amekosea. Kama Ahabu angelitenda hilo, au hao manabii wangetenda hilo, wangejiona wako makosani.

<sup>154</sup> Nabii aliyethibitishwa alisema Ahabu atakufa na mbwa watairamba damu yake. Na unabii wake ulipatana nalo. Basi alijua yuko sahihi. Hata Jehoshafati ilimpasa alione hilo na kulijua. Mikaya alipoona ono lile, hakuwa sana pamoja na wale—na hao watu katika siku hizo, lakini alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Ilikuwa sahihi.

<sup>155</sup> Angalia, twaleta jambo hili sasa katika siku hii tunapoona saa ile kuu ambayo tunajia. Angalia ambalo Daudi alikuwa akijaribu kufanya pia. Nalikuwa na maadishi madogo hapa juu ya hilo. Alikuwa akijaribu kuleta lile sanduku kwenye mji wa Daudi; dhehebu lake mwenyewe.

<sup>156</sup> Angalia nyuma kule wakati Bwana kwanza alinena kule mtoni: "Kama Yohana Mbatizaji alivyopelekwa kutangulia kuja kwa kwanza . . ." Ndugu, Waasembly hawangevumilia hilo, wala Wa-United, hao wote. Iliwalazimu wawe na mtu mahali fulani. Lo, iliwapasa wote kulitenda. Unaona? Vivyo hivyo hasa. Wote iliwalazimu walilete nyumbani kwao.

<sup>157</sup> Walitaka kulileta kwenye mji wa Daudi. Kwa sababu gani? Hapakuwepo na mahali palipokuwa tayari kwa ajili yake. Na hiyo ndiyo sababu huwezi kuuleta Ujumbe kwa dhehebu. Neno; Sanduku; Kristo, yeze yule jana, leo, na hata milele; na kufahamika Kwake kwote; huwezi kulileta kwenye dhehebu lako. Hawataliamini kamwe, kwa sababu hakuna nafasi kwa ajili Yake. Si Biblia husema kwamba alikuwa nje ya kanisa la wakati wa Laodekia akijaribu kuingia ndani? Hapakuwa na nafasi katika mji wa Daudi, haidhuru ulikuwa mwaminifu jinsi gani, na jinsi ulivyokuwa mkuu, na-na kadhalika. Bado hapakuwa na nafasi; ilikuwa iwe Yerusalem. Huko ndiko ambako lilikwenda baadaye wakati nabii alipowaambia wafanye nini na hilo sanduku. Unaona? Kwa hiyo ilimbidi Daudi kulilete katika mji wake mwenyewe. Halikuwa na mahali palipokuwa tayari.

<sup>158</sup> Kristo ndiye Sanduku letu, nao hawatampokea. Kristo ndiye Neno. Hawatalipokea. Wanapenda kanuni zao za imani, dhehebu lao, sanduku jipyaa, au—au—au gari jipyaa. Wanataka dhehebu lilibebe, sanduku jipyaa. Kumbuka Kristo ndiye Sanduku letu. Unaamini Kristo ni Neno? Hilo ndilo lile Sanduku basi. Sivyo? Sawa. Kristo hawezি kubebwa kupelekwa mahali Pake panapofaa na gari lo lote la kidhehebu. Yeye hushughulikia mtu mmoja na si kundi. Hajawahi kushughulika na kundi kamwe; mtu mmoja. Wakati Yeye . . . ? . . . Kama angefanya hivyo, Yu kinyume cha Neno Lake, Amos 3:7. Nawe huwezi kulifanya liseme uongo. La, bwana! Ni—ni kweli.

<sup>159</sup> Lakini waona, walijaribu . . . Sanduku haliwezi kubebwa na dhehebu; kuna viongozi wengi sana ndani yake. Unaona? Haiwezekani. Aliahidi hatatenda hilo, naye hatatenda. Yeye—Yeye alisema, wakati alipoahidi—wakati aliahidi kulitenda kwa njia nyingine, hiyo ndiyo sababu aliahidi hatalifanya. (Msiwazie hayo mawazo. Naweza kuyahisi. Mnaona?)

<sup>160</sup> Kwa hiyo Yeye—Yeye aliahidi angelitenda kwa njia fulani na kila kitu kinyume cha hiyo hatakifanya. Unaona? Lakini kwa njia Yake ya awali kulingana na alilosema katika Amos 3:7, hivyo ndivyo atalitenda. Na hilo lazima lithibitishwe na kuhakikishwa kuwa sahihi. Sasa, unajua nini alichoahidi leo, basi anakifanya hicho leo. Hicho ndicho tu alichosema atatenda: angefungua zile Muhuri Saba na yote ambayo angefanya; kufunua siri nyuma kule, jinsi ambavyo ubatizo huu na kadhalika ulivyokuwa umevurugwa. Na ndiyo haya hapa katika uwepo Wake hasa. Sayansi imelihakikisha. Mbingu

zimelitangaza. Binadamu amesimama, akiliangalia vizuri na kuona likitendeka. Na hamna hata jambo moja limenenwa asilofanya kweli. Naam basi. Ili tu upate kuona tulipo leo.

<sup>161</sup> Sasa, mtu ye yote aliye na roho zake anajua—ana Roho wa Mungu juu yake, anajua huu ni Ukweli; kwa sababu Roho wa Mungu hatanena kinyume cha Neno. Loo la, itapatana kabissa na Neno. Unasema, “Ninaye Roho Mtakatifu. Nilipaza sauti; nilinenka kwa lugha. Nilicheza katika Roho.” Hilo halimaanishi kitu kwa Mungu. Unaona? Daudi alifanya kitu hicho hicho—kwa kweli jambo lilo hilo nyuma kule. Waliimba kwa nguvu zake zote, naye akapaza sauti kwa nguvu zake zote; wote waliosalia walifanya hivyo, nao wanatembea moja kwa moja kuelekea mautini: Hilo ni kweli! Hilo halihusiani nalo; Neno ndilo jambo muhimu, Neno la Bwana. Wale wamnganjeao Bwana. Ndiyo, bwana.

<sup>162</sup> Unaona, wao amba wana Roho wa Mungu ndani yao huitazama ahadi ya siku ya leo, na kukesha, na kungojea mpaka waione, kisha wanasesma, “Ndiyo hiyo.” Mungu huwafunulia.

<sup>163</sup> Kama Nathanieli. Filipo alikwenda akampata Nathanieli, naye Nathanieli akasema, “Sasa, ngoja kidogo najua hilo limeahidiwa, lakini hebu nilione.” Naye alipoliona, akasema, “Ndilo hilo.”

Yule mwanamke alisema, “Sasa, najua, nimewasikiza wanatheologia wa kila namna, nimetenda *hili* na *lile*. Na nimesoma Biblia mimi mwenyewe, na najua kwamba tuna—kuna Masihi ajaye ambaye atafanya mambo haya, kwa hiyo huna budi kuwa nabii Wake.”

Akasema, “Mimi ndiye.”

<sup>164</sup> Alisema “Njoni, mmwone Mtu, hili ndilo.” Alingojea mpaka alipomwona Masihi huyo akitambulishwa na Neno la Mungu. Kisha akasema, “Huyo ndiye tumemngoja miaka mia nne. Hatujawa na nabii au cho chote. Yuko hapa, na Yeye Mwenyewe anasema kwamba Yeye ndiye. Sasa... [Sehemu tupu katika ukanda—Mh.] Njoni mmwone Mtu ambaye ameniambia mambo yale niliyotenda.” Lakini makuhani walitaka kumuua, na mwishowe walitenda. Unaona? Lakini hawawezi kuua Roho Wake leo. Hiyo ni kweli! La, hawawezi kumuua. Alikuwepo hapa kutuleta Kwake, kwa hiyo tunashukuru.

<sup>165</sup> Angalia jinsi Mungu alivyo mkuu, jinsi kazi Zake zilivyo kuu. Jinsi asivyoweza kushindwa kamwe. Sasa, Mungu ana njia iliyoandalialiwa na ya asili ya kufanya mambo, naye hatatenda kinyume cha hiyo.

<sup>166</sup> Sasa, aliahidi katika siku za mwisho kile ambacho angetenda. Na aliwapelekeaa—sisi Ujumbe, na Ujumbe huu ungekuwa na utambulisho ule ule aliokuwa nao kama uliokuwa na Eliya, kama uliokuwa na Elisha, kama ulivyo kuwa na Yohana Mbatizaji. Na utageuza miyo ya watu, si kuelekea dhehebu,

lakini kuelekea kwa wale baba wa asili na wa kimitume, kurudi kwenye Neno. Jinsi mambo haya yalivyothibitishwa. Jinsi katika kutolewa kwa sauti ya malaika wa mwisho, Ufunuo 10: Katika siku za malaika wa saba siri hizi zote ambazo... Kwa nini Wamethodisti walifanya hili, na Wabatisti, na Church of Christ, na Mashahidi wa Yehova, wote hufanya hilo? Hizo siri zitafunuliwa katika siku za mwisho wakati wale malaika saba—Ujumbe wa malaika wa saba, wakati yeye, si wakati atakapoanza kufanya hili, lakini atakapoanza kutangaza Ujumbe wake. Unaona? Si miaka ile ya maandalizi, lakini ule—wakati atakapoanza kutangaza Ujumbe, siri hizi basi zitafunuliwa. Na ndizo hizi hapa, bila kuzijua, na ninyi watu ni shahidi wa hilo. Na kisha katika kituo kile cha kuchunguzia anga—ili ulimwengu usitilie shaka—bado wanashangaa kumetokea nini.

<sup>167</sup> Huko Tucson hivyo vituo vikubwa vyta kuchunguzia anga walichukua picha yake kule juu, bado wangali wakishangaa nini ilitendeka. Ni nini? Bado wangali wanayaandika magazetini, “Kuna mtu ye yote anayejua cho chote kuihusu? Nini, jinsi iliviyotendeka?” Hakuna ukungu huko juu; hakuna hewa, hakuna unyevu, maili thelathini juu angani. Loo, jamani! “Kutakuwa na ishara katika mbingu juu. Na mambo haya yatakapotendeka, matetemeko ya nchi mahali mahali, ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni.” Siku hiyo (Luka) Mwana wa Adamu atajifunua tena, na awe amefunuliwa Mwenyewe. Na ulimwengu utaonekana kama Sodoma na Gomora. Loo, jamani, ndugu, msiwe wajinga wa mambo ya kiroho. Mnaona? Yachunguzeni Maandiko kwani katika hayo mnafikiri—mna uzima wa Milele, na hayo ndiyo yanayoshuhudia Neno. Hayo ndiyo yanayoishuhudia ile Kweli, mambo ambayo Mungu anatenda katika saa hii.

<sup>168</sup> Na sasa, angalia! Hao walio na Roho wa Mungu hungojea mambo haya. Na wanapoonaa mambo hayo, huamini mambo hayo. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba (Yeye ni Neno), watakuja Kwangu—watakuja Kwangu.”

<sup>169</sup> Nimekuwa mkali sana asubuhi hii. Unoana? Wanamngojea Bwana, kungojea; na wangojeapo, huona ahadi ile ya siku ya leo ikithibitishwa, huifanya upya imani yao katika Neno Lake, sababu aliahidi kulifanya, na yuko hapa akilitekeleza. Basi hakuna shaka. Mungu hunena; Neno Lake kwanza hunena, kisha Roho yule anayelileta anatenda kitu kile ambacho Neno lilisema angetenda. Loo, tuna maigizo mengi sana. Bado tutakuwa nayo mengi, mtu mwenye moyo mwaminifu akijaribu kufanya jambo njia *hii* na njia *ile*, lakini angalia kilichotokea. Watu wataweka mikono yao, na kisha—kisha wafe. Unaona?

<sup>170</sup> Angalia, hakuna mipango ya binadamu ya kidhehebu itakayotenda kazi. Wakijitengenezea wanachama kwa sanduku

lao la madhehebu waliloitengenezea . . . Mungu kamwe hajawa na dhehebu. Kamwe hatakuwa na dhehebu. Na ni kitu kilichotengenezwa na binadamu.

<sup>171</sup> Nami leo nashangaa kama katika kuwavuta kwetu kote na mikutano mikubwa na ufuluo mwangi, kama hatukuwa tukijaza sanduku la Kimethodisti, sanduku la Kibatisti, sanduku Kipresbeiteria. Vipi Sanduku la Kristo Neno? Na kama Bibi-arusi anapaswa kuwa Neno, basi yampasa—na kuwa wa Kristo, sehemu ya Bwana Arusi, yampasa awe Neno, Neno si kwa siku Yake, Neno la siku hii ambalo aliahidi litatimia siku hii. Alisema amepeleka Neno Lake kumfinyanga Bibi-arusi Wake na kumtengeneza. Natumaini tunalionia. Usiweke mawazo yako mwenyewe sasa, na usichukue wazo la mtu mwagine. Chukua Neno lillothibitishwa hapa, Biblia. Linasema . . .

<sup>172</sup> Mungu ameahidi katika Neno Lake jinsi ambavyo angechagua Bibi-arusi Wake katika siku ya mwisho. Ulijua hilo? Alilahidi, jinsi ambavyo angelifanya, na hilo kwa mpango Wake wa awali wa kumchagua Kristo, wa kuchagua wakati, kuchagua majira jinsi yeye . . . Hawezi kulikosa katika Bibi-arusi Wake, kwa sababu Yeye ni sehemu ya Neno lile. Hawezi kulichagua kwa dhehebu na huku hakumchagua Kristo kwa dhehebu. Kristo alikuja kupitia dhehebu? Alilijilia dhehebu? La! Walimkataa. Vema, hicho ndicho madhehebu yalifanya basi; ndipo amchaguapo Bibi-arusi, anaweza kuja kwa njia nyingine? Alimletaje Kristo hapa? Kwa Neno la manabii. Sivyo? Angeleta Bibi-arusi Wake hapa jinsi gani? Kwa Neno la manabii. Alimtambulishaje alipokuja? Kwa mtu aliyekuwa na roho ya Eliya juu yake akitokea jangwani. Atamtambulishaje Bibi-arusi Wake? Aliahidi katika Malaki 4 kitu kile kile kabla ya kuiharibu dunia kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.

<sup>173</sup> Kumbuka, Sodoma iliteketazwa. Hili ni kweli? Vema, dunia hii itateketezwa. Yesu alisema hivyo. Na itakuwa wakati ambao—kama Luka sura ya 17 na mstari wa 30 ilivyosema: Katika siku zile itakuwa kama Sodoma na Gomora, kisha Mwana wa Adamu atafunuliwa. Na basi nini kingetokea? Kulingana na Malaki, atateketeza dunia tena, nao wenye haki katika ule Utawala wa miaka Elfu watatembea katika majivu ya waovu. Sivyo? Unaona? Kwa hiyo tuko katika wakati wa mwisho kabisa. Tumeketi hapa mlangoni sasa tukimngojea aje.

<sup>174</sup> Angalia, Mungu aliahidi katika Neno Lake kwamba atachagua Bibi-arusi Wake kwa njia yake ya awali aliyomchagua Bwa—Bwana Arusi Wake. Alilitabiri kwa manabii na akamtuma nabii kumtambulisha. Nabii alisema akitokana katika kingo za Jordani, “Tazama!”

Walisema, “Wewe ni Masihi, sivyo?”

Alisema, “La, mimi siye Masihi.”

“Hunabudi kuwa Masihi yule.”

<sup>175</sup> “Lakini Mimi siye, lakini anasimama kati yenu. Na viatu Vyake, sistahili kuvifungua. Ajapo, hujitambulisha Mwenyewe...” Na leo anasimama kati yenu katika Umbo la Roho Mtakatifu, akijidhihirisha Mwenyewe zaidi na zaidi, akija katika Kanisa Lake, akijulisha Mwenyewe; kwa sababu Yeye na Bibi-arusi, na Bwana Arusi, watakuwa kitu Kimoja, akijulisha Mwenyewe: Na siku moja utaona ya kwamba yule ambaye ulimhisi moyoni mwako na kuona utambulisho Wake, atafanyika mwili mbele yako. Kisha wewe na Yeye ni Mmoja. Na mmeunganishwa na Neno, kisha Neno lililokuwako hapo mwanzo litarudi mwanzo ambaye ni Mungu. “Na siku ile ninyi mtatmbua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Haleluya! Tumewasili! Haleluya! Ninafurahi sana kumuona ye ye akijifanya mwili kati yetu na kuona kile alichoahidi kwa Neno, si misisimko ya mtu fulani, kuimba na kuruka, na kucheza, lakini kwa Neno Lake (amina!) Anajifanya ajulikane.

<sup>176</sup> Angalia walipoleta—na kujenga hekalu na kuliingiza lile sanduku ndani yake, Mungu aliingga humo na Nguzo ya Moto. Amina! Ilikuwa Daudi akiruka na kupiga kelele za furaha. Ilikuwa waimbaji wote na makuhani wakisherehekea huku wakiwa nje ya mapenzi ya Mungu. Lakini Mungu alipoliona lile sanduku katika mahali na sehemu Yake, kabla hawajaliingiza lile sanduku mle ndani, hapa ikaja Nguzo ya Moto ikiongoza njia, moja kwa moja juu ya mbawa za makerubi na moja kwa moja nyuma ya patakatifu pa patakatifu, mahali pake pa kupumzikia, Nguzo ya Moto. Na utukufu wa Mungu ulikuwepo ndani mle hadi...?...hawakuona jinsi ya kuhudumu. Amina! Itafunga macho ya kila mtheologia atakapokuja kumchukua Bibi-arusi Wake. Atachukuliwa juu u—usiku wa manane, kama ilivyokuwa, kwao. Hata hawatamuona akienda. Lo, sifa ziwe kwa Mungu!

<sup>177</sup> Angalia. Mungu aliahidi kwamba angemwondoa Bibi-arusi Wake, lile angetenda: Patakuwa na mbegu; kutakuweko Nuru wakati wa jioni, ambavyo angetenda haya mambo yote, sawa kabisa, na kwa njia ambayo alipanga awali katika Agano la Kale na Agano Jipy—a si kupitia katika madhehebu. Si kupitia mipango yetu tunayotumia leo. Tunasababisha mauti. Weka... watu wana—wanaliwekea mikono yao nao hufa kwa sababu hiyo. Unaona?

<sup>178</sup> Neno, Ujumbe wa jioni lazima uwe na matokeo ya jioni. Ujumbe wa jioni lazima upande mbegu za jioni, si za asubuhi, mbegu ya jioni. Sivyo? Tukio la saa sita—mbegu zake nyuma kule zilikuwa dhehebu. Likafa, likaangamia. Lakini Ujumbe wa wakati wa jioni utaonyesha Nuru ya wakati wa jioni, utaonyesha matokeo ya jioni. Ujumbe wa wakati wa jioni... wakati wa Yesu, ule ujumbe wa adhuhuri ulionyesha matokeo ya adhuhuri. Ujumbe wa mwanzo ulionyesha matokeo ya

mwanzoni: ulifanya maumbile. Alimfanya Mwanawe katika Sura Yake adhuhuri. Wakati wa jioni anatengeneza Bibi-arusi kwake. Unaona? Kwa nini? Neno Lake. Alitengenezaje dunia? Aliitamkaje ikatokea? Kwa Neno Lake! Mwanawe alikuwa nani? Neno! “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu...Naye Neno alifanyika mwili akakaa...” Atachukuaje Bibi-arusi Wake? Kwa Neno, sio kwa gari jipya, si kwa wazo la mwanatheologia, lakini kulingana na Neno Lake atamtambulisha. Usiweke kitu kimoja katika hilo au kuondoa kitu kimoja toka hilo sasa. Liache jinsi lilitivyo. Unaona?

<sup>179</sup> Wakati wa jioni, aliahidi atafunua—atafunua hizi Muhuri Saba na kuonyesha yale ambayo makanisa yalikuwa yamekosa nyuma kule. Ufunuo 10, na Malaki 4, Luka 17:30, alisema atalifanya, kwa hivyo tusilichanganye. Hebu tuliweke moja kwa moja hivyo.

<sup>180</sup> Hebu katika kufunga...Ni kama, karibu kabisa saa sita kasorobo; hebu nifunge katika kusema hili. Rafiki zangu, sikilizeni katika Jina la Bwana Yesu, mambo haya ni wazi sana kwenu kutokuyaamini. Ni wazi sana kwenu kutokuyaona. Hakika mnaweza kuona hayo. Hakika ulimwengu unaweza kuyaona. Lakini...Sasa, usishawishiwe na huu umaridadi wa upuzi na mambo waliyo nayo leo. Sijali ni watu wazuri namna gani, jinsi walivyo waaminifu, ikiwa hawasemi sawa sawa na sheria na manabii, Biblia ilisema hawana Uzima ndani yao. Unaona?

<sup>181</sup> Daudi alifikiria alikuwa sahihi; alikuwa mwaminifu. Hao makuhani walifikiria walikuwa sahihi; walikuwa waaminifu. Lakini walishindwa tu kumtaka shauri Bwana kuhusu hilo. Nao wangalilifanyaje hilo? Labda walisema, “Tuliomba sana.” Lakini hiyo haikuwa njia ya Mungu ya kulifanya. Aliahidi kwamba hatafanya neno mpaka kwanza awafunulie watumishi Wake manabii. Na hapo alikuwa amesimama Nathanieli kati yao, na kamwe hawakumtaka shauri.

<sup>182</sup> Sasa soma sura chache zinazofuata za Mambo ya Nyakati hapo, nawe utaona wakati Daudi alipoketi katika nyumba ile na kusema, “Ni sawa (Nathanieli alikuwa ameketi pamoja naye) kwamba nikae katika nyumba ya mierezi na—na sanduku la Mungu linakaa chini ya hema huko nje. Naye Nathanieli akapata kutoka kwa Bwana jambo la kumwambia afanye.

<sup>183</sup> Naye alikuwa amekosea, kwa hiyo Mungu alisema, “Mwambie mtumishi wangu Daudi, ninampenda. Nilimfanya jina kama watu wakuu duniani, lakini siwezi kumruhusu alitende (Waona?); alinikosea. (Waona?) Sitamruhusu alitende. Nitamleta mtu: mwanawe atainua nyumba ya milele ya Mungu.” Na huyo alikuwa Daudi bila shaka. Ambaye Sulemani alikuwa mfano wake, lakini basi alishindwa. Kila mtu lazima hana budi kushindwa. Kila mwanadamu hana budi kushindwa. Mungu

ndiye pekee ambaye hawezi kushindwa. Hawezi kushindwa. Hilo ni jambo moja ambalo Mungu hawezi kufanya, ni kushindwa. Na Mungu ni Neno. Na Neno . . . Haidhuru ionekaneje lazima lije njia hii nyingine, litakuja jinsi hasa Neno lilivyosema.

<sup>184</sup> Sasa kumbuka, yakupasa ufuate majira, muda. Unaona? Na majira unayoishi, wakati gani, na kuthibitisha hilo kuona kwamba ni Kweli kabisa.

<sup>185</sup> Sasa chukua lazima hizi zote, Neno lote, mifano yote, na mambo yale, kisha angalia unapokaa. Fikiria juu ya wakati tunaoishi. Angalia kule ng'ambo ya kwamba karibu moja asili kumi ya dunia iko tayari kuzama. Sayansi inasema hivyo. Wanaangalia saa. Miaka michache iliyopita walisema, "Ni usiku wa manane kasoro dakika tatu tu." Huenda ikawa ni dakika moja; huenda ikawa ni nusu dakika sasa.

Walisema, "Halitatendeka katika kizazi chetu."

<sup>186</sup> "Yaweza kutendeka mnamo dakika tano." Na angalia, jambo jingine alilosema, "Miaka mitano" Sikusema hilo sasa, Yeye alisema hilo, yule mwanasayansi. Wanasongamana kutoka California kama inzi. Unaona? Vema, siku ile Lutu aliyotoka Sodoma, siku ile ile ilinyesha mvua ya moto juu ya nchi. Mojawapo ya siku hizi Mungu attachukua Ujumbe wetu, nasi tutaondoka hapa. Kitu fulani kitatokea bila shaka, Kanisa litakapoondoka, Mwili Wake, Bibi-arusi Wake.

<sup>187</sup> Sasa, nataka kuwasomea Andiko, na nawataka mlisome pamoa nami. Nataka mfungue katika kumbukumbu la Torati 4 katika kufunga. Nafikiri ya kutosha labda yamekwisha nenwa mpate kuelewa. Kumbukumbu la Torati 4. Nitasoma mahali pawili humu ndani. Na kwa kanisa hili, na kwenye kanda—watu wanaosikiza kanda, na watu katika sehemu zilizounganishwa kwa redio wanaosikiza nchini kote, nawatakeni msikilize hili kwa makini na msikose. Hili ni jambo ambalo mimi . . . Kumbukumbu la Torati sura ya 4, sasa, nitaanza mstari wa kwanza. Nataka kusoma msitari wa kwanza, kisha nitasoma mstari wa 25 na 26. Mwaweza kusoma yote mtakapofika nyumbani, lakini kuokoa tu muda ili tupate kuondoka katika wakati, sababu sina budi kurudi tena usiku wa leo, Bwana akipenda. Sikilizeni akinena nabii huyu. Alikuwa katika uwepo wa Mungu. Alijua ambalo alikuwa anazungumzia. Sikilizeni:

*Na sasa, Ee Israeli, zisikilizeni amri na hukumu niwafundishazo, ili mzitende; mpate kuishi na kuingia na kumiliki nchi awapayo BWANA, Mungu wa baba zenu. (Hilo ni mfano wa ule Utawala wetu wa Miaka Elfu.)*

*Msiliongeze neno niwaamurulo, wala msilipunguze, . . . (Msiongeze kitu kimoja kwenye hilo na msipunguze kitu kimoja toka kwa hilo, kaeni, semenii*

*tu lisemavyo.) . . . mpage kuzishika amri za BWANA, Mungu wenu, niwaamuruzo.*

*Macho yenu yameona aliyoyatenda BWANA . . . kwa sababu ya Baal-peori; maana watu wote waliomfuata Baal-peori, BWANA, Mungu wako, amewaangamiza kutoka kati yako. (Sasa, ninyi ni wateule kutoka katika madhehebu hayo. Mnaona, mnaona?)*

*Bali ninyi mlionambatana na BWANA Mungu wenu, mnaishi kila mmoja wenu hata leo. (Hamkufa pamoja na madhehebu yenu; mnaishi sasa na katika uwepo wa Mungu. Kwa kufunga usilikose.)*

Msitari wa ishirini na tano sasa wanapoingia nchini mle, sasa angalia kitakachotendeka.

*Utakapozaa wana, wana wa wana, na mki . . . mkisha kuwa katika nchi siku nyngi, mkajaribu wenye, . . . (Hilo ndilo lilitendeka.) na kujifanya . . . sanamu za kuchonga . . . (kitu kingine) . . . au kwa umbo la kitu cho chote, mkafanya ambayo ni maovu machoni pa BWANA, Mungu wako, na kumtia hasira: (Sikilizeni!)*

*Nawashuhudizia mbingu na nchi hivi leo, . . . (Mnaona?) . . . kwamba karibu mtaangamia kabisa juu ya nchi . . . au mahali . . . ambapo mwivukiayo Jordani kuimiliiki; hamtafanya siku zenu ziwe nyngi juu yake, ila mtaangamizwa kabisa.*

<sup>188</sup> Huyu alikuwa Musa akinena na Israeli baada ya ye ye kuthibitishwa na Mungu kwa Nguzo ya Moto na kujuu alithibitishwa kuwa mtumishi wa Mungu kuwaongoza watoke. Na kabla hawajakwenda katika nchi ile, kabla hawajaingia, Musa alisema, “Sasa maneno niliyonena kwenu, naita mbingu na nchi kushuhudia dhidi yenu. Mkiongeza kitu kimja kwake au kuondoaa neno moja toka kwake, hamtagumu katika nchi awapayo Bwana Mungu.” Nasema vivyo hivyo katika Jina la Yesu Kristo. Usiongeze kitu. Usiondoe—kuliwekea mawazo yako. Wewe sema tu yaliyosemwa katika kanda hizo. Tenda sawasawa kabisa na vile Bwana Mungu amekuamuru kutenda. Usiongezee Kwake.

<sup>189</sup> Yeye kama kawaida, hutimiza ahadi Yake kwetu. Kila ahadi aliyotoa ameitimiza. Aliwaambieni yatakayotendeka, na je, yalitendeka? Nazileta mbingu na nchi mbele yenu leo kuwahimiza, Mungu aliwahi kusema cho chote ambacho hakutimiza na kutenda sawasawa na alivyosema angetutendea? Ametenda sawasawa hasa na alivyosema angetenda? Hilo ni sawa hasa! Ataendelea kufanya vivyo hivyo. Usiliongezee. Usilipunguzie. Liamini tu nawe utembee kwa unyenyekevu mbele ya Bwana Mungu wako, kwani tunakaribia kuingia katika nchi ile. Ndipo hutarudi. Hutarudia maisha kama haya tena. Utarudi kama kiumbe kisichokufa. Utarudi dhambi

itakapokuwa imeondolewa, Shetani atakapofungwa. Na kwa miaka elfu moja utaishi juu ya nchi hii ambayo Bwana Mungu wako amekupa. "Maana wapole watairithi nchi. Heri yeze azitendaye amri Zake zote, ili aweze kuwa na haki ya kuingia katika Mji ule, kwani huko nje wako wachawi, waongo, wazinzi, na mbwa; hawataingia humo." Ni kwa waliokombolewa tu na kwa wale waendao katika amri Zake.

<sup>190</sup> Usichukue kitu kipyaa. Vinaruka kila mahali, na kutakuwa na zaidi ya hayo yatakayokuja. Lakini usichukue mambo haya mapya. Bwana Mungu wako amekutangazia yaliyo Kweli. Bwana Mungu Wako amethibitisha Kweli ni nini kwa Neno Lake na kwa Roho Wake. "Si kwa uweza, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho Yangu." Na Roho... Mungu anawatafuta wale ambao wanamwabudu katika Roho na Kweli. "Neno Lake ni Kweli." Na amethibitisha vizuri kabisa kwamba Yesu Kristo ni yeze yule jana, leo, na hata milele. Amewaonyesha ninyi mbegu za jioni. Ameifunua kwenu katika Neno. Amethibitisha hilo kwenu kwa Roho Wake.

<sup>191</sup> Msianzishe au kujaribu kuunda dhehebu kamwe. Msijaribu kujenga juu ya kitu cho chote kingine, lakini dumuni wanyenyekevu mbele za Bwana Mungu wenu, kwani yaonekana kama malango huenda yakafunguliwa ya kuingia katika nchi ya ahadi hivi karibuni. Basi natuingie kwa kuimba kwa kweli na shangwe, wakati Bibi na Bwana Arusi wanapochukua mahali pao kwenye kiti cha enzi.

<sup>192</sup> Ishini wanyenyekevu; ishini wenye kupendana. Pendaneni. Msiringize kamwe kitu kati yenu. Ukiiona kitu kinakuja moyoni mwako dhidi ya mtu fulani, kitoe papo hapo. Usimuachie... Na Shetani atafanya awezavyo kuingia kati yenu. Mnaona? Msiache hilo litokee. Mtu fulani mwenye ulimi laini huenda akaja akakutoa katika hilo. Unafikiri waliweza kumshawishi Musa atoke katika uwepo wa Mungu ambapo alikuwa amesimama pale na kuliona? La, bwana! La, hatulipunguzi au kuliongeza! Liwekeni tu vile ambavyo Bwana alisema. Hatutaki dhehebu; hatutaki vyama. Hatutaki uovu; hatutaki fitina; twamtaka Mungu; naye ni Neno. Sasa na tuinamishe vichwa vyetu.

<sup>193</sup> Ee Mungu, naangalia huku na huko na jicho la kiroho; najaribu kuona kinachotendeka. Naona Neno Lako, namna lilivyothibitishwa, namna lilivyohakikishwa. Siku zote toka miaka thelathini na mitatu, hapa mtoni, ulivyo sema, na lipo hapa miaka thelathini na mitatu baadaye, na unatenda ulilosema tu. Na umetenda ulilonena tu. Bwana, jambo hili na liwe mbali nasi kujaribu kulifanya dogo au kujaribu kulifanya kubwa. Niliweke tu vile ulivyolitengeneza. Nitembee kwa unyenyekevu na kukufuata Wewe.

<sup>194</sup> Hawa ndio wao, Bwana, ambao umewatoa kwa huduma mbali na wale wanalala nchini, pande zote za dunia. Makaburini

hana yanashikilia wengi wa wale wanaongoja, watakatifu waliobarikiwa. Lakini ni kama ilivyosema; sisi tulio hai, tuliosalia, hatutawatangulia wao waliolala. Parapanda italia, nao waliokufa watafufuliwa kwanza, kisha tutanyakuliwa pamoja nao. Utukufu wa Mungu utakapokuwa duniani, utalificha Kanisa toka kwa ulimwengu. Hata hautalionia liendapo.

<sup>195</sup> Baba Mungu, waweke hawa mikononi Mwako. Ni wako. Naomba, Mungu, kwamba siku zote tutatembea kwa unyenyekevu mbele Zako. Hatujui ni muda gani; Hatuna hamu ya kujua ni muda gani; Si kazi yetu. Ni kazi Yako. Si mapenzi yetu kujua utakujua lini; ni mapenzi yetu, Bwana, kuwa wanyenyekevu hata utakapokuja, na kutembea pamoja Nawe. Tunataka sana Wewe kujithihirisha mara kwa mara, Baba, kati yetu, tupate kuona kwamba bado twatembea pamoja nawe.

<sup>196</sup> Tusamehe dhambi zetu zilizopita. Tuongoze na utulinde na kila mtego wa ibilisi kwa ajili ya siku zijazo. Tuongoze na utulinde, ee Mungu, Baba yetu. Tusamehe dhambi zetu na utusaidie kuwa watoto Wako. Tu watu wa tabaka maskini. Tu waliokataliwa na watu wa dunia hii, na madhehebu ya makanisa. Tunaona mwisho, na tunakushukuru kwa kuona kwa jicho la kiroho katika Neno Lako kuona wakati wa mwisho. Kwani mambo yote haya lazima yafikie kule kupigwa kwa mawe kukuu toka Mbinguni. Tusaidie, Bwana, tusiwe hapa siku ile, lakini tuwe tumekwenda katika uwepo Wako, kuruka hadi kifuani Mwako.

<sup>197</sup> Ponya wagonjwa na wanaoteseka Bwana. Twaomba ya kwamba usiku huu utatupa ibada kuu. Twaomba kusiwe na mtu mnyonge mionganii mwetu kwa sababu ya Uwepo Wako, Bwana. Miyo yetu na ikuelekee Wewe daima. Na twajua, Bwana, kwamba fedha, mali, mambo ya ulimwengu hayana maana, ni ya muda tu. Yote lazima yatoweke. Kazi zetu, mahali petu, rafiki zetu, kila kitu hakina budi kuondolewa. Haidhuru tu matajiri, tu maskini, tunapendwa au hatupendwi jinsi gani, yote hayana budi kuondolewa. Lakini kuna kitu kimoja tu hapa ambacho ndio kiini cha kuwepo kwetu humu, na hicho ni Yesu Kristo. Kwa hivyo, Mungu, hebu na tuweke kando kila kitu ambacho si cha maana na kushikilia Yeye, naye ni Neno. (Tujalie, Bwana) Neno lililotabitishwa la saa hii.

<sup>198</sup> Neno lililotabitishwa la siku za Musa lilikuwa Yesu. Neno lililotabitishwa la siku za Isaya, Eliya, Yohana, wote, lilikuwa Yesu. Na Neno lililotabitishwa leo ni Yesu, ye ye yule jana, leo na hata milele. Tusaidie, Bwana, kuamini hilo, kuona hilo, na kutembea ndani yake. Tu—tunaomba katika Jina la Yesu.

<sup>199</sup> Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nataka kujua kama kuna wengine ndani hapa ambao kamwe hawajafikia ile hatua kuu inayotosheleza... Unaliyamin hilo, lakini kuliyamin tu

hakutoshi. Naamini kwamba mke wangu alikuwa msichana mzuri. Nilimjua baba yake, mama yake. Nilimjua kwa miaka na miaka. Aliishi maisha yaliyonyoka. Ninaamini alikuwa mwanamke mzuri, lakini hilo halikumfanya wangu. Hakuwa wangu mpaka yeye—nilipomkubali, aliponikubali. Sasa Yesu anataka kukubali. Hutamkubali na kuwa sehemu ya Neno Lake? Kama hujafanya hilo, huku vichwa vyenu vimeinamishwa na miyo yenu imeinamishwa, natumaini . . .

<sup>200</sup> Hakuna nafasi kwa mwito wa madhababuni hapa. Siamini sana hiyo kwa vyo vyote. Naamini Mungu hukuzuru papo hapo ulipo. Nyosheni mikono yenu, mseme, “Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi. Nataka kufanya hilo.” Mungu akubariki. Mimi . . . Mungu akubariki. Jamani, mikono kila mahali. Nataka kuwa hivyo. Mungu akubariki, Ndugu, Mungu akubirika Ndugu wote mlion hapa. “Nataka kuwa hivyo.” Mungu abariki . . . “Kwa kweli nataka kuwa hilo.” Na—naliona . . . Vema sasa, tazama, rafiki, huenda kukawa na kitu kidogo . . . kama tu hilo, basi, kuna kitu fulani kimekuwa kiini chako mbali na hilo. Uko karibu sana nacho, unakiangalia. Unakiona. Umekiona kwa miaka kadhaa kikisogea. Unakiona kikikomaa sasa. Kama hilo linamaanisha kila kitu kwetu na hakuna kitu kingine kitakachodumu isipokuwa Hicho, kwa nini usikipe kisogo kitu hicho ulichokuwa ukiangalia na kuweka moyo wako Kwake, ambaye ni Kiini cha maisha yote ya hapa baadaye ni Yeye. Mbona usifanye hilo wakati tunaomba pamoja?

<sup>201</sup> Mungu mpenzi, hapo pana mikono ya wanaume, wanawake, wavulana, wasichana, hata wahudumu, wameinua mikono yao juu. Wao—walitaka ku—kusema kwamba walitaka kiini chao kiwe ni Bwana Yesu, na bado inaonekana kama hawawezi kulitenda; kuna kitu kinawavuta *hivi* na *vile*: Huenda ikawa ni dhehebu; huenda ikawa ni mtu, huenda ikawa ni dhambi; huenda ikawa ni kitu wanachoficha moyoni mwao. Sijui, Bwana; Wewe unajua. Hata iwe ni nini, na iwe hivi, Bwana, unapoita wengine . . . Umekwisha waita; Ni wako. Na wakati unawaita, na waachilie hiyo—hiyo dhambi inayowasumbua, kama Biblia ilivyosema “Na tuweke kando kila mzigo mzito na dhambi ile ituzingayo kwa upesi, ili tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu.” Tukimtazama nani? Kazi yetu? Dhehebu? Jamii yetu? Halmashauri? Kristo, Mwenye kuazisha na Mwenye Kutimiza imani tuliyo nayo katika Yeye. Tenda hilo, Baba, kwa ajili yetu leo. Kwani tunaomba hilo katika Jina Lake na kwa utukufu Wake.

<sup>202</sup> Sasa, ni Wako, Bwana; tenda nao kama uonavyo yafaa. Tenda nasi kama uonavyo yafaa; tu Wako. Katika Jina la Yesu. Amina.

Ni nampenda, ninampenda,  
Kwa kunipenda kwanza,  
Kaninunulia wokovu  
Kalvari.

<sup>203</sup> Mmesahau chakula cha jioni? Mmesahau kama watoto wote ni salama kule nje katika gari au la? Mmesahau yote kuhusu wakati uliopita na kutambua hicho unachokisikia ni nini sasa? Kinafanyika mwili mbele yako siku kwa siku. Unaona? Acha hilo liwe kiini cha lo lote... Acha mambo yaliyosalia yaondoke; yataangamizwa kwa vyo vyote. Lo, endelea tu kumfuata. Kama Elisha alivyomfuata Eliya, na tumfuate. Kwani nasi lazima tutwaliwe juu pia siku moja. Tumeona gari la moto ambalo lilimtoa kaburini. Tunalihisi kati yetu sasa. Siku moja ataenda kufungulia farasi vijitini. Tunaenda juu. Mtampenda?

Kaninunulia wokovu  
Kalvari.

Loo, huwezi karibu kabisa tu—kufumba macho yako na umwone Yeye akining'inia kule?

Ninampenda, (Nimpende mwengine yupi?)  
Ninampenda,  
Kwa kunipenda kwanza,  
Kaninunulia wokovu  
Kalvari.

<sup>204</sup> Kila wakati ninaporudi nyumbani, mtu fulani amekwisha kuaga dunia. Nitaondoka miezi michache, nirudipo, mtu fulani ameaga dunia. Ninapatwa na huzuni kila wakati njapo. Hivi majuzi mvulana tulisoma shulen i naye, alipokuwa akija barabarani alisema, "Hujambo, Billy."

<sup>205</sup> Nilimtazama; alikuwa ni kijana mdogo mwenye sura nzuri, nywele nyeusi zinazometameta zimechanwa kuelekea nyuma. Sasa, ni nyeupe kama theluji. Alikuwa amenyoka sana; na ana kitambi hivi. Nilisema, "Hujambo, Jim." Nilimuangalia; nikamsikitikia; nilifikiri, "Mungu, mimi na mvulana huyo, mimi na mtu yule tuna umri mmoja." Basi najua siku zangu zimehesabiwa. Najua si muda mrefu sana uliosalia. Ninaangalia pande zote, nafikiri, "Nifanyeje, Bwana? Nisaidie. Sitaki kukutangulia. Nataka nidumu moja kwa moja—moja kwa moja nyuma Yako. Wewe ongoza njia. Nami naangalia, nafikiri, "Miaka hamsini na sita, loo, jamani, haujasalia muda mrefu sana." Nami naangalia chini, namuona rafiki yangu mzuri Bill Dauch akikaa pale, miaka sabini na miwili sabini na mitatu.

<sup>206</sup> Naangalia pande zote; nawaona watoto hawa wakifikiria, "vema, nitangojea mpaka niwe mzee kama Ndugu Branham, nitawazia hayo..." Mpenzi, inawezekana usilione hilo; naona shaka sana kwako kuliona hilo. Unaona? Lakini hebu fikiria tu, kama Ndugu Bill Dauch akimaliza siku hii, ataishi zaidi ya mamia ya watu wenye umri wa miaka kumi na mitano, kumi na sita. Wanakuwa kila saa. Kwa hivyo kuna tofauti gani una umri gani? Unafanya nini kuhusu saa unayoishi. Unamfanya nini Yesu wakati huu? Unaona? Loo, nataka kumwona Yeye. Nataka kuona saa ile nitakapoiona miili hii

yote hii mizee imebadilishwa, kuwaona wamebadilika katika muda wa kufumba na kufumbua. Kama hilo sivyo, basi sisi ni watu wapumbuvu kuliko wote; kuleni, kunyweni na mfurahi kwani kesho mnakufa. Mnaona? U kama mnyama tu; unakufa na kuingia katika takataka na hayo ni mwisho. Lakini kuna isiyokufa—nafsi isiyokufa inayoishi ndani yako, ndugu. Tumekwisha sikia toka Mbinguni. Tumekwisha liona likithibitishwa. Tunajua Yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii.

<sup>207</sup> Sasa, enyi washiriki wa Mwili wa Kristo, tunapoliiimba hilo tena nawatakeni mketi katika viti vyenu na kupeana mikono tunapoimba hilo tena.

Ninampenda, (Msalimie tu ndugu yako, dada)  
ninampenda,  
Kwa kunipenda kwanza, (Richard!)  
Kaninunulia wokovu.  
Kalvari.

<sup>208</sup> Mnampenda, semeni, "Amina!" [Kusanyiko linajibu "Amina!"—Mh.] Mnalipenda Neno Lake, semeni "Amina!" [Kusanyiko linajibu, "Amina"—Mh.] Mnapenda ushirika Wake, semeni, "Amina! [Kusanyiko linajibu, "Amina!"—Mh.] Mnapenda mwili Wake, semeni, "Amina!"] [Kusanyiko linajibu, "Amina!—Mh.] Basi pandaneni! Amina. Hilo ni kweli. "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."

<sup>209</sup> Sasa, nimeweka mikono yangu juu ya vitambaa hivi kama itawalazimu kuwa navyo kabla ya usiku... Nitamuomba Ndugu Richard Blair, Mungu alijibu sala yake, yeye na ndugu yule mwingine, hapo akiomba hivi majuzi kumrudisha huyu mvulana mdogo ambaye anaketi kati yetu leo, ambaye anaishi kwa sababu ya imani yao katika Mungu... Na sasa, nitamuomba aturuhusu tuondoke katika neno la maombi katika muda mchache tu ujao, ili tuweze kuja tena usiku huu. Ni kama saa sita na dakika tano kwa saa ile. Nami nawatakeni mrudi usiku huu, kama mkiweza, kama mpo. Kama huna budi kwenda nyumbani, Mungu na akupe safari njema barabarani, na akusaidie, na akulinde. Kama waweza kubaki na unataka kubaki, unakaribishwa kubaki hapa. Mungu awe pamoja nanyi sasa.

Hata twonane huko juu,  
Hata (Hebu tuinue mikono yetu kwa...)  
twonane Kwake kwema,  
Hata twonane huko juu,  
Mungu awe nanyi daima.  
[Ndugu Branham anaanza kuugugumiza  
wimbo uo huo—Mh.] (Hiyo ndiyo njia ya  
kuondoka katika nyumba ya Mungu, kwa

maombi, kwa unyenyekevu, tukitumaini tutakutana tena usiku huu. Kama hatukutani, Mungu awe nanyi) hata tutakapoonana tena . . .

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Ndugu Blair.



*KUMTENDEA MUNGU KAZI BILA MAPENZI YAKE SWA65-0718M*  
(Trying To Do God A Service Without Being The Will Of God)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Julai 18, 1965, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)